Nipashe
Jumamosi Juni 27, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0580269
The Guardian digital
www.ippmedia.com
nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710

Albinism Hotline
• Jifunze kuhusu Ualbino
• Toa taarifa za nia ovu dhidi ya wenye Ualbino
0800 75 00 50
Piga simu bure
HAKI YETU PROJECT
UNDER THE SAME SUN
215779502



# Polisi waua 2 tuhuma ujambazi na kunasa mtandao wizi magari

UKURASA 3

## BAA LA CORONA



Kaa nyumbani na ujitenge hata kama una dalili ndogo za Covid 19 kama kukohoa, kuumwa kichwa na kusikia homa mpaka utakapopata nafuu. WHO

- Nawa mikono kwa sabuni na maji yanayotiririka
- Epuka kusalimiana kwa kushikana mikono na kukumbatiana
- Ukipiga chafya au kukohoa, ziba mdomo

# Serikali yatoa maelekezo ulipaji ada shule binafsi

- Wanafunzi wenye pumu, selimundu marufuku kuvaa barakoa...

*Endelea Uk. 2*



Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako

# TAKUKURU ILIVYOOKOA MAMILIONI YA MSTAAFU

UKURASA 3




Scan Hapa
Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu
Google Play
App Store


# Mtoto wa tatu wa Rais achukua fomu Zanzibar

UK. 3

**MICHEZO** MWAMNYETO AFUNGUKA KUSUASUA KWA COASTAL UK.23

MAONI, KATUNI UK.6

HABARI KITAIFA

# Maelekezo ada shule binafsi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WIZARA ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imetoa maelekezo ya ulipaji ada kwa shule binafsi na kuziagiza Kamati na Bodi za shule kufanya uchambuzi wa gharama inayopaswa kupungua kwa siku ambazo wanafunzi hawakuwa shuleni kutokana na janga la corona.

Pia, Wizara imeagiza wanafunzi wote kupokelewe na kuendelea na masomo bila kikwazo chochote ili kukamilisha muhula.

Maelekezo hayo yalitolewa jana na wizara hiyo kupitia taarifa iliyotolewa na Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano serikalini wa wizara hiyo, Sylvia Lupembe, kwa vyombo vya habari.

Katika taarifa hiyo, Lupembe alisema kamati na bodi hizo zinatakiwa kufanya uchambuzi wa malipo ya chakula na usafiri na tathmini hiyo izingatie ratiba mpya ya mihula iliyotolewa na wizara.

"Kulingana na Sheria ya Elimu sura namba 353 iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2002, uendeshaji wa shule unasimamiwa na kamati au bodi za shule, vyombo ambavyo vimeundwa kwa mujibu wa sheria hiyo,"alisema.

Aliwataka wamiliki wa shule kuzingatia sheria hiyo na kuzipa nafasi bodi kutekeleza majukumu yake kulingana na matakwa ya sheria.

Alisema wizara inaelekeza wanafunzi wote wapokelewe kwa ajili ya kuendelea na masomo ifikapo Juni 29, mwaka huu na kusisitiza kusiwapo na nyongeza yoyote ya ada.

"Kulingana na ratiba iliyotolewa na wizara, wanafunzi wanatarajia kukamilisha masomo kama inavyoelekezwa na mihtasari ya madarasa waliyopo, hivyo ada za shule zilipwe kulingana na makubaliano yaliyoafikiwa mwanzoni mwa mwaka wa masomo,"alisema.

Kadhalika, wazazi wanatakiwa kuzingatia kiwango cha ada kukadiriwa kwa kuzingatia gharama mbalimbali za uendeshaji wa shule, ambazo ziliendelea kuwapo hata muda ambao shule zilikuwa zimefungwa.

"Gharama hizi ni pamoja na mishahara ya watumishi, ankara za umeme na maji," alisema.



Watoto wa kitongoji cha Kiembeni, kata ya Mapinga wakivuka kwenye daraja lililotengezwa kwa miti na mbao bila ya kuweka kingo za pembeni katika Mto Mapinga, wilayani ya Bagamoyo, mkoani Pwani jana, kitendo ambacho ni hatari kwa wavukaji. **PICHA: MIRAJI MSALA**.

# 'Wanafunzi wenye pumu na selimundu wasivae barakoa'

**Na Romana Mallya**

SERIKALI imetoa mwongozo mpya wa afya kwa shule, vyuo na taasisi za elimu na kutaja mambo makubwa manne ya kuzingatiwa ili kujikinga na virusi vya corona.

Vilevile, mwongozo huo unawataka wanafunzi chini ya miaka minane na wale wenye matatizo ya mfumo wa hewa kama vile pumu; matatizo ya moyo; na selimundu wasivae barakoa.

Mwongozo huo uliotolewa jana na Waziri wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, pia unataka kuhakikisha kunakuwa na mazingira salama kabla ya wanafunzi kurejea shuleni Jumatatu.

"Endapo wataumwa na kukosa pumzi, waepuke mikusanyiko, wavue barakoa kuongeza kiwango cha hewa na watafute msaada wa wataalamu wa afya," Ummy alisema katika taarifa yake ya mwongozo huo akirejea wanafunzi wenye matatizo yaliyotajwa.

Waziri Ummy pia uliutaka uongozi wa shule uhakikishe wanafunzi wote wakati wa kufanya mazoezi, ikiwamo kukimbia mchakamchaka, hawatakiwi kuvaa barakoa.

"Siku ya kwanza ni muhimu itumike kutoa elimu kwa wanafunzi, wafanyakazi, wasaidizi wa wanafunzi wa watu wenye ulemavu kuhusu corona pamoja na dalili zake," alisema.

Waziri huyo alisema kuwa katika kuandaa mazingira, wanatakiwa kutakasa mazingira yote ya shule ikihusisha shule ambazo zilitumika kutunza washukiwa au wagonjwa wa corona na hilo lifanyike angalau saa 72 kabla ya wanafunzi kuingia.

Pia, shule na vituo vimetakiwa kuwa na vifaa vya kunawia mikono katika kila eneo au maeneo ya madarasa, ofisi, lango kuu, bweni, maktaba, bwalo la chakula na kwenye vyoo.

"Tunasisitiza matumizi ya sabuni na maji tiririka ndiyo iwe njia kuu ya usafi wa mikono. Spiriti (Methanol) isitumike kama kitakasa mikono katika maeneo yote ya shule au chuo. Wanafunzi wasiagizwe kwenda navyo," alionya.

Waziri Ummy alisema uongozi wa shule, vyuo na vituo uhamasishe wanafunzi, walimu na wafanyakazi wao, wakiwamo wasaidizi wa wenye ulemavu, kuvaa barakoa za vitambaa wakati wanaporudi shuleni.

Aliagiza wazazi au walezi wahimizwe kuwapatia watoto wao barakoa za vitambaa kabla ya kwenda shuleni na ikitokea kukawa na dalili, taarifa zitolewe ili wafanyiwe vipimo kabla ya kurudi shuleni.

Pia, alisema kwa watakaotumia magari ya shule, wamiliki wahakikishe kunakuwa na vitakasa mikono kwa ajili ya wanafunzi wakati wa kupanda kuelekea shuleni na wahudumu wavae barakoa.

"Watakaopanda daladala, utaratibu wa sasa wa usafiri utatumika ambapo kila mmiliki wa basi la abiria anawajibika kutii maelekezo ya usalama wa abiria," alisema.

Kadhalika, alisema kwa watoto wadogo kwenye shule za awali, vituo vya kulelea, wanatakiwa kusaidiwa kwenye unawaji wa mikono kama inavyotakiwa.

Alisema kwa shule, vyuo na vituo vyenye wanafunzi wenye mahitaji maalumu, walimu wanapaswa kuvaa barakoa maalum zitakazoruhusu mwanafunzi mwenye matatizo ya usikivu kuwasiliana nao.

Waziri Ummy aliwataka wataalamu wa afya wa mikoa na halmashauri mara kwa mara wafanye ukaguzi kwenye shule zilizoko katika maeneo yao, ili kuhakikisha tahadhari zote za kujikinga zinazingatiwa kabla na wakati wa masomo.

# Mtoto mwingine wa rais achukua fomu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MTOTO wa Rais mstaafu wa pili Zanzibar, Mussa Aboud Jumbe, ameongeza idadi ya watoto wa marais wastaafu kisiwani hapa kuchukua fomu ya kutaka kumrithi Rais anayemaliza muda wake, Dk. Ali Mohamed Shein.

Idadi ya watoto wa marais wastaafu waliochukua fomu hizo mpaka sasa imefikia watatu baada ya Jumbe kuchuka jana.

Waliokwisha kuchukua na kurudisha ni Balozi Ali Karume, ambaye ni mtoto wa Rais wa kwanza na Dk. Hussein Ali Mwinyi mtoto wa Rais wa tatu wa Zanzibar.

Jana saa 8:27 mchana, Jumbe ambaye ni Mkurugenzi wa Uvuvi, alifika katika ofisi za CCM Kisiwandui kuchukua fomu za kuingia kwenye kinyang'anyiro hicho na kufikisha idadi ya walioonyesha nia ya kugombea nafasi ya urais kuwa watu 30.

Waonyesha nia 30 waliochukua fomu hizo, 14 kati yao wamerudisha jana wakiwamo Profesa Makame Mbarawa Mnyaa na Shamsi Vuai Nahodha.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya kurejesha fomu hiyo, Shamsi Vuai Nahodha, alisema mchakato wa uchukuaji wa fomu kwake ni mzuri hasa kwa wadhamini ambao walikuwa wakijitokeza kutaka kumdhamini.

Kwa upande wake Profesa Makame Mbarawa, alisema hakuna changamoto yoyote iliyojitokeza katika uchukuaji na urejeshaji wa fomu kutokana na chama kuweka utaratibu mzuri katika zoezi hilo.

"Tunakishukuru chama hasa kwa uongozi kuhakikisha wanasimamia jambo hilo kwa umakini na umahiri mkubwa,"alibainisha.

Aliwaomba Watanzania kuendelea kumuombea na kusubiri uamuzi wa chama katika vikao vyake vitakavyofanyika mwezi ujao.

Waonyesha nia 29 waliochukua fomu hadi jana ni Mbwana Bakari, Balozi Ali Karume, Mbwana Mwinyi Yahya, Omar Shehe, Muhammed Jafar, Muhammed Hija, Meja Jenerali Issa Suleiman Nassor, Shamsi Vuai Nahodha, Dk. Hussein Mwinyi, Profesa Makame Mbarawa, Mwatum Mussa Sultan, Haji Rashid Pandu, Dk. Abdul-halim Mohammed Ali, Jecha Salim Jecha na Dk. Khalid Salum Muhamed.

Wengine ni Rashid Ali Juma, Khamis Mussa, Mmanga Mjengo Mjawiri, Hamad Yussuf Masauni, Muhammed Aboud, Bakari Rahid, Ibrahim Makungu, Ayoub Muhammed Mahmoud, Hashim Salum Hashim, Hasna Ataai Maoud na Fatma Kombo Masoud, Pereira Ame Silima, Iddi Hamad Iddi na Shaame Ame Silima, Mussa Aboud Jumbe.

HABARI KITAIFA

# Takukuru ilivyyookoa mamilioni ya mstaafu

**Na Renatha Msungu,**

DODOMA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) mkoani Dodoma, imeokoa Sh. milioni 10 za mafao ya mstaafu Frida Nahamani, ambazo alidhulumiwa na taasisi ya kukopesha ya Swahili Trust.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini hapa, Mkuu wa Takukuru Mkoa wa Dodoma, Sosthenes Kibwengo, alisema taasisi hiyo ilimzidishia marejesho ya mkopo wake wa Sh. milioni 15 alizokopa.

Alisema taasisi hiyo inayomilikiwa na Maswe Mgaya ikifanya biashara ya ukopeshaji, ilibainika katika uchunguzi wa Takukuru kuwa kati ya Julai hadi Desemba 2018, kumkopesha mstaafu huyo Sh. milioni 15.

"Baada ya kupewa mkopo, alikabidhi kadi yake ya benki kwa taasisi hiyo ili warejeshe fedha zao mara mafao yake ya kustaafu yakitoka. Hata hivyo, mstaafu alipor ejeshewa kadi yake Januari 31 mwaka 2019, alikuta akaunti yake haina fedha yoyote ilhali alipokea mafao zaidi ya Sh. milioni 46," alisema.

Kiongozi huyo wa Takukuru alifafanua kuwa baada ya uchunguzi wa Takukuru, wamejiridhisha taasisi hiyo ilizidisha kiasi cha Sh. milioni 10 kwenye makato.

"Fedha hizi zimerejeshwa baada ya Takukuru Mkoa wa Dodoma kuingilia kati na kuwataka kufanya hivyo," alisema.

Katika hatua nyingine, Takukuru imeokoa Sh. milioni 74.2 za vyama vya akiba na mikopo (Saccos) vya Mwashita na Duwasa ambazo zilikuwa mikononi mwa wanachama 32 waliokuwa na madeni kwa muda mrefu.

Kibwengo pia alisema Sh. milioni 9.3 za vitambulisho vya wajasiriamali zimeokolewa kutoka kwa watumishi 37 katika Halmshauri ya Chamwino.

"Pia, tumekusanya vitambulisho 270 vyenye thamani ya Sh. milioni 5.4 ambavyo vilikuwa mikononi mwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Chamwino, lakini pia awali tulifanikiwa kuokoa Sh. milioni 7.2 na vitambulisho 105 katika Wilaya ya Kongwa, Bahi, na Mpwapwa ambapo fedha hizo ziliingizwa katika akaunti za Makatibu Tawala wa wilaya na Wakurugenzi wa halmashauri," alisema.

Wakati huo huo, watu wawili, akiwamo Mtaalamu wa Maabara ya Kituo cha Afya Kwamtoro wilayani Chemba, Bakari Mayegeye na Mjasiriamali Mwanaidi Mshana, wamekamatwa kwa tuhuma za ubadhilifu wa mali ya umma.

"Mshana alikamatwa na maofisa wa Takukuru jijini Dodoma akiwa na makasha yenye vifaa tiba ambavyo ni mali ya serikali na baada ya kuchunguza, wakabaini kwamba alipatiwa na Mayegeye ambaye alivichukua kinyume cha taratibu za kituo cha kazi," alisema.

Alisema wawili hao wamekuwa wakishirikiana kuiba na kuuza kwenye maduka ya dawa ya watu binafsi jijini Dodoma na wilayani Chamwino.

Alisema vifaa tiba hivyo vilipaswa kutolewa bure katika hospitali hizo na kwamba hatua stahiki zitachukuliwa dhidi yao mara baada ya uchunguzi kukamilika.

## Polisi waua wawili tuhuma ujambazi

**Na Waandishi Wetu**

JESHI la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, linawashikilia watu watano kwa tuhuma za wizi wa magari jijini humo ambayo mara baada ya kuyaiba huyauza mikoa mitatu ya Mwanza, Shinyanga na Geita.

Vilevile, jeshi hilo limewaua watuhumiwa wawili wa ujambazi katika matukio mawili tofauti na kukamata silaha walizokuwa wakizitumia kufanikisha uhalifu wao.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini jana, Kamanda wa Kanda hiyo, Lazaro Mambosasa, aliwataja watuhumiwa wa vitendo vya wizi wa magari kuwa ni: Hatibu Mwinyi (35), mkazi wa Katoro, Geita; Onesfori Venance maarufu Massawe (28), mkazi wa Kimara; Jabir Rajabu (40) mkazi wa Nyamanoro Mwanza; Sanford Hezekia (41), mkazi wa Nyakato Mhandu Mwanza; na Nasir Said (44), mkazi wa Bushushu Shinyanga.

INAENDELEA UK. 4

TRA
MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA
Imethibitishwa na ISO 9001: 2015

OFISI ZA TRA KUWA WAZI JUMAMOSI NA JUMAPILI NCHI NZIMA

*Dar es Salaam 25 Juni, 2020:*

Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) inapenda kuutaarifu Umma kuwa, ofisi za TRA nchi nzima zitakua wazi siku ya **Jumamosi** tarehe **27 Juni, 2020** na **Jumapili 28 Juni, 2020** kwa ajili ya kutoa huduma kwa walipakodi kuanzia **saa 2:30 asubuhi** hadi **saa 11:00 jioni.**

WOTE MNAKARIBISHWA!

*"Pamoja Tunajenga Taifa Letu"*

Imetolewa na;

**Idara ya Huduma na Elimu kwa Mlipakodi**
**TRA MAKAO MAKUU**

215791502

# Ashtakiwa kusafirisha gramu 1523 dawa za kulevya

**Na Hellen Mwango**

MFANYABIASHARA Pedro Chongo, maarufu Salum Mgana, amepandishwa kizimbani katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu akikabiliwa na mashtaka ya kusafirisha pipi 90 za dawa za kulevya aina ya cocain zenye uzito wa gramu 1523.25 na thamani ya zaidi ya Sh. milioni 76.

Mshtakiwa huyo alisomewa mashtaka yake mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Richard Kabati.

Wakili wa Serikali, Janeth Magoho, alidai kuwa Aprili 9, 2011 katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere, Chongo alikutwa akisafirisha pipi 90 za dawa za kulevya zenye uzito na thamani iliyotajwa.

Magoho alidai upelelezi wa kesi hiyo bado haujakamilika na aliomba tarehe nyingine ya kutajwa kesi hiyo. Mshtakiwa hakutakiwa kujibu chochote kwa sababu mahakama hiyo haina uwezo wa kusikiliza kesi hiyo.

Hakimu Kabati alisema kesi hiyo itatajwa Julai 10, mwaka huu na mshtakiwa apelekwe mahabusu.



Mjumbe wa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya CCM Taifa na Mlezi wa CCM Mkoa wa Dar es Salaam, Makamu wa Rais Samia Suluhu Hassan, akisalimiana na wananchi na baadhi ya Wajumbe wa Kamati ya Siasa na Sekretarieti ya CCM Wilaya ya Kinondoni, alipowasili katika Ofisi ya DMDP Magomeni jana, kwa ajili ya kuzungumza na Wajumbe wa Kamati ya Siasa na Sekretarieti ya CCM, akiwa katika ziara ya kichama mkoani Dar es Salaam. **PICHA: OMR.**

# Gharama maonyesho Sabasaba zafyekwa

**Na Mary Geofrey**

NAIBU Waziri wa Viwanda na Biashara, Stellah Manyanya, amesema Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara (TanTrade), imepunguza gharama za viingilio kwa wafanyabiashara wadogo kwenye maonyesho ya biashara ya Sabasaba.

Awali, wajasiriamali waliokuwa wanaingiza biashara zao katika maonyesho hayo, walikuwa wakitozwa Sh. 300,000, lakini sasa watatozwa kuanzia Sh. 150,000.

Manyanya aliyaeleza hayo juzi jijini Dar es Salaam, alipotembelea na kukagua maandalizi ya Maonyesho ya Kimataifa ya 44 ya Biashara na kusema lengo kuwa ni kuwashawishi wajasiriamali kujitokeza kwa wingi.

Alisema wamefikiria kupunguza gharama hizo kutokana na kuwapo kwa janga la corona lililosababisha hali ya uchumi kuyumba hasa kwa wafanyabiashara wadogo.

"Kwa kutambua kuna wafanyabiashara ambao wameteterekа kutokana na kuwapo kwa janga la Covid-19, hivyo tumewaangalia na kuweka punguzo kidogo ili kuwawezesha waje waonyeshe bidhaa zao," alisema Manyanya.

Kadhalika, alisema kwa wafanyabiashara wasio na uwezo wa kulipa Sh. 150,000, nao wataendelea kuwafikiria.

Kuhusu wafanyabiashara wakubwa, Manyanya alisema gharama hazitapungua kwa sababu lengo lao ni kuhamasisha wajasiriamali kujitokeza kuonyesha bidhaa zao.

Alibainisha kuwa hadi juzi, jumla ya kampuni 3,600 (sawa na asilimia 75) zimeshajitokeza kushiriki maonyesho na kwamba matarajio ni kuwa wataendelea kujitokeza kwa wingi.

Alisema pia watakuwa na maonyesho kwa njia ya mtandao ambayo yatahusisha bidhaa za nafaka kama mahindi na mchele.

Manyanya alisema kuwa katika maonyesho hayo, wataanzisha mikutano kati ya wazalishaji wa kahawa na katani kwa ajili ya kubadilishana mawazo na watu wa teknolojia.

# Kiwanda chatoa ajira zaidi ya 200

**Na Mohab Dominick,** KAHAMA

WANANCHI 250 wameajiriwa katika Kiwanda cha Kahama Plastic Investment, mkoani Shinyanga kinachozalisha viroba vya kuhifadhia mazao ya nafaka.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kiwanda hicho, Khamis Mhoja, aliwaambia waandishi wa habari kuwa lengo la kuanzisha kiwanda hicho katika Wilaya ya Kahama ni kuunga mkono juhudi za Rais John Magufuli kufikia uchumi wa kati kupitia viwanda na kuisaidia serikali kutoa ajira kwa wananchi.

Aliahidi kudumisha uhusiano kwa wananchi wanaozunguka kiwanda chake kwa kutoa ajira nyingi na kuongeza kuwa mpaka sasa asilimia 60 ya wananchi wanaozunguka kiwanda hicho wameajiriwa.

Alisema kiwanda hicho huchukua mifuko chakavu inayookotwa mitaani kama malighafi na pia ni njia moja ya kusafisha mazingira ya Mji wa Kahama.

"Kwa sasa kiwanda kimewashwa kwa majaribio, tulikwamishwa na ugonjwa wa homa ya mapafu unaosababishwa na virusi vya corona, matarajio yetu ni kuzalisha tani tano kwa siku," alisema.

Alisema mifuko iliyotupwa majalalani wanaiokota na kurejesha kiwandani ili kutengenezwa upya. Soko la bidhaa hiyo limelengwa Kanda ya Ziwa ambayo ina wakulima wa mazao mbalimbali yanayohitaji vifungashio hivyo.

Wakazi wa eneo hilo, Debora Nyanda, Neema Lukumo pamoja na Khamis Isa, walisema kuanzishwa kwa kiwanda hicho kumewasaidia kupata ajira na kujiingizia kipato cha kukidhi mahitaji yao na familia zao tofauti na hapo awali.

"Kwa kweli kuanzishwa kwa kiwanda hiki sisi kama wanawake wa eneo la Mhongolo tumepata fursa ya ajira ukilinganisha wengine tuna fani ya ushonaji kwa kutumia cherehani, tulikuwa hatuna ajira, lakini kwa sasa tunapata riziki kidogo," alisema Neema.

# Polisi waua wawili tuhuma ujambazi

INATOKA UK. 3

Alisema watu hao walikamatwa katika msako wa kuwatafuta wezi wa magari uliofanyika kati ya Mei 28 hadi Juni 13 mwaka huu.

"Wamekutwa na magari matano ambayo yaliibwa na kupelekwa mikoa hiyo mitatu ambayo ni T 425 DQE aina ya Toyota Kluger, T 162 DBU Toyota Harrieh, T 423 CFF, Toyota Noah, T 761 CVL Toyota Town ACE na T 999 DDF Toyota IST, walioibiwa magari yao wajitokeze kuyatambua," alisema.

Katika hatua nyingine, jeshi hilo limewaua watuhumiwa wa ujambazi wawili na kupata silaha mbili aina ya bastola.

Kamanda Mambosasa alisema mtuhumiwa wa kwanza aliuawa Juni 19, usiku maeneo ya Mbangala Zakhem baada ya polisi kupata taarifa za ujambazi uliotaka kufanyika huko kwenye maduka ya miamala ya fedha.

Alisema watuhumiwa wa ujambazi wapatao watatu kabla ya kufanikisha azma yao hiyo, walibaini kuwapo kwa makachero ndipo walipofyatua risasi na katika majibizano, jambazi mmoja alipigwa risasi ya mgongoni na kufariki papo hapo.

Alisema watuhumiwa wenzake walifanikiwa kukimbia na kutokomea kusikojulikana na upekuzi uliofanywa kwa marehemu alikutwa na bastola aina ya Browning yenye namba A 953749 na TZCAR 101379 ikiwa na risasi tano ndani ya kasha.

Kamanda Mambosasa alisema tukio la pili lilitokea Juni 13, usiku maeneo ya Shekilango karibu na bandari kavu ambapo kikosi kazi cha kupambana na ujambazi, kikiwa kinawafatilia majambazi watatu waliokuwa kwenye pikipiki, ghafla kilishambuliwa.

"Katika mashambulizi hayo, polisi walijibu mapigo na kumjeruhi kwa risasi mmoja kati ya majambazi hao na alifariki dunia wakati akipelekwa hospitali.

"Alipopekuliwa, alikutwa na bastola aina ya Rivolver iliyotengenezwa Brazil yenye namba J.006703 ikiwa na risasi nne ndani ya kasha," alisema.

Alisema miili yao imehifadhiwa Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (MNH) na juhudi za kuwatafuta majambazi waliokimbia zinaendelea.

***Imeandikwa na Fatuma Mtutuma na Romana Mallya***

## Viongozi Zuya AMCOS watuhumiwa ubadhirifu

**Na Happy Severine,** SIMIYU

KAMATI ya Udhibiti na Usimamizi Tume ya Maendeleo ya Ushirika, imemtaka Mrajisi msaidizi vyama vya ushirika mkoa wa Simiyu kwa kushirikiana na Ofisa Ushirika halmashuari ya Mji wa Bariadi, kuwachukulia hatua waliotumia vibaya mali za chama cha msingi cha ushirika Zuya.

Viongozi wa Zuya AMCOS wanatuhumiwa na wanachama kwa matumizi mabaya ya mali za chama ikiwamo fedha.

Wakiongea mbele za wajumbe wa kamati hiyo, wanachama hao walidai kuwa baadhi ya viongozi wamekula pesa zao walizochanga kwa ajili ya hisa.

Walidai pamoja na pesa za hisa kuna za viingilio vya wanachama ambazo pia hazionekani na matumizi mabaya ya mapato ya chama yatokanayo na ushuru wa pamba.

"Tumekuwa tukihoji kitabu cha hisa muda mrefu hakionekani, tuliunda kamati ikaonekana pesa zetu za hisa alichukua mmoja wa viongozi, watu wamekula pesa za viingilio, wamegawana pesa za ushuru ambazo ni mapato ya chama," alisema Elia Elisha.

Wanachama hao waliomba msaada kutoka kwa wajumbe wa kamati hiyo kuwachukulia hatua viongozi wao ambao wamehusika katika ubadhilifu huo ikiwamo wa kuchukua mali za chama kama mashamba.

Ofisa Ushirika wa halmashuari hiyo, Billwalter Mbilinyi, alisema ofisi yake imeanza kuwachukulia hatua baadhi ya viongozi baada ya kubaini malalamiko ya wanachama yana ukweli.

"Tulifanya uchunguzi na kubaini ubadhilifu wa baadhi ya mali na fedha, wote waliohusika walikamatwa na wameanza kurejesha pesa hizo kwa makubaliano maalumu," alisema Mbilinyi.

Mrajisi wa Mkoa Ibrahimu Kadudu, alisema wameendelea kuwachukulia hatua viongozi wote waliohusika na wizi katika vyama na kwamba kwa mwaka huu jumla ya kesi nne za uhujumu uchumi zimefunguliwa dhidi ya viongozi hao.

"Tumekuwa tukitumia njia za busara kuwataka waliotumia mali za vyama warejeshe kama ni pesa au vingine, lakini sasa hivi tunaenda mbele zaidi kuwafikisha mahakamani, hata hapa Zuya tutawachukulia hatua," alisema Kadudu.

Robert Busuma, mjumbe wa kamati hiyo na Kamishna wa tume hiyo, aliwataka Mrajisi na Ofisa ushirika huyo kuhakikisha mali zote za chama hicho zinarudishwa na wahusika wanachukuliwa hatua.

# Wanne mbaroni tuhuma rushwa kuwania ubunge

**Na Said Hamdani,** LINDI

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) mkoani Lindi, inawashikilia watu wanne, akiwamo mtia nia wa nafasi ya ubunge, Ally Chinumba (CCM), kwa madai ya kuwashawishi wajumbe wa Halmashauri Kuu ya Kata wampitishe kwenye kura za maoni.

Naibu Mkuu wa Takukuru mkoani hapa, Charles Mulebya, alitoa taarifa za kukamatwa kwa watuhumiwa hao alipozungumza na waandishi wa habari ofisini kwake jana.

Alisema Chinumba alikamatwa juzi Nahukahuka, Jimbo la Mtama saa 11 jioni alasiri wakati yeye na wajumbe wasiopungua (23) wa Halmashauri ya Kata hiyo, nyumbani kwa Ally Chinumba, ambaye ni baba mzazi wa mtia nia huyo.

Mulebya alisema Chinumba ambaye pia ni mtumishi wa Shirika la Ugavi wa Umeme (Tanesco) makao makuu jijini Dar es Salaam, alikutwa akiwa amewakusanya wajumbe hao kwa lengo la kuwashawishi wampitishe kwenye kura za maoni, ili kugombea kwenye kinyang'anyiro cha ubunge mwaka huu Jimbo la Mtama.

Alisema kwenye gari la mtia nia huyo lenye namba za usajili T.527 DEY (hakutaja aina ya gari) maofisa wa Takukuru walikuta fedha kiasi cha Sh. 841,000 zilizokuwa zimewekwa maeneo tofauti tofauti, zikiwamo bahasha ndogondogo dazani moja zinazohisiwa zimeandaliwa kwa ajili ya kuwekea fedha kwa ajili ya wajumbe husika.

"Gari la mtia nia tulipolipekua, tumekuta fedha Sh. 841,000 na dazani moja ya bahasha ndogo ndogo, bila shaka zilikuwa za kuwekea fedha za wajumbe," alisema.

Alipoulizwa kama wajumbe waliowakuta wanawashikilia, kiongozi huyo wa Takukuru alijibu kuwa wanawashikilia watu wanne akiwamo mtia nia husika, lakini hakuwa tayari kuanika majina ya watuhumiwa wengine watatu.

Alisema Takukuru inaendelea na uchunguzi ili kubaini uvunjifu wa sheria, kwa mgombea huyo kujihusisha na vitendo vya kushawishi wajumbe kwa utaratibu wa kutoa rushwa.

Aliwaonya watia nia wote kwa nafasi mbalimbali zikiwamo za ubunge na udiwani kujihusisha na vitendo vya rushwa, akiwataka wafuate utaratibu, kanuni na sheria zilizowekwa.



Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Maridhiano Taifa, Askofu Oswald Mlay, akizungumza na wanachama wa jumuiya hiyo wa wilaya ya Ilala, jijini Dar es Salaam juzi, kuhusu maandalizi ya kongamano kubwa la kuombea amani kuelekea katika uchaguzi mkuu litakalofanyika Agosti 23, mwaka huu, katika uwanja wa Jamhuri Jijini Dodoma. **PICHA: MUHIDINI MSAMBA**.

# Ujio MV Victoria kutoa fursa wana-Kagera

**Na Allawi Kaboyo, BUKOBA**

WANANCHI mkoani Kagera na maeneo jirani wametakiwa kujiandaa na fursa zitakazojitokeza baada ya meli ya MV Victoria hapa kazi tu, kuanza safari zake za Bukoba-Mwanza baada ya kukamilika ukarabati kwa asilimia 98.

Akitoa taarifa ya ujio wa meli hiyo jana katika mkutano na waandishi wa habari mjini hapa, Mkuu wa Mkoa wa Kagera, Brigedia Jenerali Marco Gaguti, aliwataka wananchi mkoani humo kujiandaa kwa biashara na safari za kwenda Mwanza kwa kuwa mkombozi anarejea.

Alisema meli hiyo itaanza kufanyiwa majaribio ya safari ndefu kutoka jijini Mwanza na bandari ya Bukoba Juni 28, 2020 na haitaruhusiwa kubeba abiria bali mizigo zaidi ya tani 100. Aliwataka wenye mizigo kujitokeza kwa kuwa wakati wa kurudi Mwanza itasafirishwa bure.

"Wananchi mkoani hapa jitokezeni kwa wingi ili kuipokea meli yenu inayotarajia kuanza safari yake ya majaribio Jumapili (kesho), ujio wa meli hii ni mapinduzi makubwa ya usafiri na usafirishaji katika Ziwa Victoria chini ya serikali katika kuchochea uchumi wa wanaKagera na Watanzania kwa ujumla," alisema.

Pia, aliongea na waendesha bodaboda kuhusu ujio wa meli hiyo na kuwataka wajiandae kufanyakazi ya kusafirisha abiria pamoja na mizigo katika kipindi cha ujio wa meli hiyo.

Abdusalum Mashankala, Mwenyekiti wa waendesha pikipiki Manispaa ya Bukoba, alisema ujio wa meli hiyo utaongeza mzunguko wa fedha kwa bodaboda hao kwa kuwa wasafiri watakuwa wengi na kuwataka kujiandaa na fursa hiyo.

Meneja wa Mamlaka ya Bandari, Bulenge Ndalo alisema mpaka sasa maandalizi ya kuipokea meli hiyo yanaendelea vizuri ikiwamo kuboresha miundombinu ya majengo na ofisi pamoja na kujenga ghala la kutunzia mizigo huku akiwaomba Watanzania hasa wanaKagera kuja kuwekeza katika biashara kwenye maeneo ya bandari.

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# *Waamuzi ongezeni umakini Ligi Bara ikielekea ukingoni*

**LIGI** Kuu Tanzania Bara leo inatarajia kuingia katika raundi ya 31, kwa timu 16 kushuka dimbani kuwania pointi tatu kwenye viwanja nane hapa nchini.

Ligi hiyo ndio ya juu na hutoa mwakilishi wa Tanzania Bara katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika, hivyo wahusika wote wanatakiwa kuongeza umakini wakati wanaposhiriki mechi za ligi hiyo.

Mechi za ligi hiyo ambayo zinatarajiwa kuchezwa leo ni kati ya Yanga dhidi ya Ndanda, Ruvu Shooting itaikaribisha Namungo wakati Alliance itawavaa Coastal Union huku Mtibwa Sugar ikiwa ugenini kwa Mwadui FC mkoani Shinyanga.

Biashara United yenyewe itawakaribisha Azam FC, Mbeya City itawakabili JKT Tanzania, Singida United inayoburuza mkia itawaalika Lipuli FC na Kagera Sugar itavaana na KMC.

Ligi hiyo itaendelea tena kesho Jumapili kwa 'Maafande' wa Tanzania wakiwaalika mabingwa watetezi na vinara, Simba huku Mbao FC iliyowahi kufundishwa na Mrundi Etienne Ndayiragije ikiwakaribisha Polisi Tanzania.

Hata hivyo wakati ligi hiyo inayodhaminiwa na Kampuni ya Simu za mikononi ya Vodacom ikielekea lala salama, katika kila raundi kumekuwa na malalamiko yanayowahusisha waamuzi.

Lakini kama haitoshi, baadhi ya wadau wamekuwa na rekodi, waamuzi kuonekana kuzipendelea baadhi ya timu na hivyo, kudaiwa kama makosa hayo yanafanywa kwa sababu maalumu, nazo ni kuzipendelea timu husika.

Wiki iliyopita, Azam FC iliamua kupelekea malalamiko yake katika Bodi ya Ligi, ikilalamika waamuzi kuwaonea katika mchezo wao dhidi ya Yanga kwa kuwanyima mabao mawili ya wazi kwa kutafsiri wafungaji waliotea kabla ya kufunga na baadaye kuwanyima penalti iliyotokana na mchezaji wake kuangushwa ndani ya eneo la 18.

Leo malalamiko ya Azam, mabingwa watetezi wa michuano ya Kombe la FA linaweza kupuuzwa, kwa sababu inafahamu ilishaondoka kwenye mbio za ubingwa, lakini je kama bado ingekuwa kwenye vita ya kuwania taji hilo au ikisaka pointi za kujinusuru na janga la kushuka daraja, mambo yangekuwa mabaya zaidi.

Nipashe inawakumbusha waamuzi kuongeza umakini kwa sababu mechi zilizobakia ni chache na kila timu imejipanga kurekebisha makosa waliyofanywa wakati msimu unaanza na hivyo kila timu ivune ilichopanda.

Umakini wa waamuzi utasababisha kila timu ipate matokeo inayostahili baada ya filimbi ya mwisho kupulishwa na kuacha kukumbuka machungu ya 'uamuzi' mbovu au wa upendeleo ulioonekana katika mechi husika.

Waamuzi watakavofanya kazi yao kwa weledi, itasaidia timu itakayotwaa ubingwa kupata taji hilo kwa haki, lakini kwa upande wa Ligi Kuu Tanzania Bara, vita hiyo sasa imehamia kwenye klabu zinazopambana kujiepusha na janga la kushuka daraja.


Kutokana na kanuni mpya za msimu huu, timu nne zitashuka moja kwa moja, na mbili zitacheza mechi za mtoano, hivyo mpaka sasa bado hakuna anayefahamu hatima yake kwa timu ambazo zina pointi chini ya 42.

Tunawakumbusha waamuzi na wasimamizi wao kuendelea kuwakumbusha maofisa hao kufanya kazi yao kwa kiwango cha juu ili msimu wa Ligi Kuu Tanzania Bara umalizike kwa amani.

Mbali na Ligi Kuu, pia waamuzi hao, wanatakiwa pia kuendelea kutafsiri vema sheria 17 za soka pale watakaposimama katikati kuchezesha mechi za michuano ya Kombe la FA, ambayo pia hutoa tiketi ya kushiriki mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Kumbukeni kufanya vizuri katika mechi za hapa nchini, kutasaidia kuwapa nafasi ya kuchezesha mechi za kimataifa, kwa sababu wanaonekana mubashara sehemu mbalimbali duniani.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# *Asiyekubali kushindwa si mshindani*

Na Barnabas Maro

**MTU** asiyekubali kushindwa si mshindani. Methali hii hutumiwa kuwanasihi binadamu wakubali wanaposhindwa au kukiri udhaifu wao.

Wahenga walitwambia: "Kweli ingawa chungu niambie usinifiche." Maana yake niambie ukweli hata kama una uchungu. Methali hii yatufunza umuhimu wa kuwa na tabia ya kusema kweli au kuwa watu wasemao kweli.

Nimeona michezo ya Azam, Simba na Yanga ambazo ndizo timu kubwa nchini. Nakumbusha jinsi Azam ilivyocheza na Yanga Jumapili iliyopita na mchezo uliotangulia kati ya Simba na Mwadui ya Shinyanga, Simba iliposhinda kwa mabao 3-0.

Kwa maoni yangu, jinsi timu za Simba, Azam na Yanga zilivyo kwenye Ligi Kuu inayoelekea ukingoni, nathubutu (ingawa naumia moyo) kusema; kama jinsi zilivyo kwenye nafasi zake sasa, ndivyo zilivyo kwa namna zinavyocheza uwanjani.

Najua kuna watakaobisha. Wacha wabishe kwani kila mtu ana mtazamo na vionjo vyake. Ni dhahiri kuwa Simba wanajua kuumiliki mpira. Inapendeza jinsi wachezaji wanavyopasiana mpira uwanjani bila papara na namna wanavyofanya mashambulizi dhidi ya timu pinzani.

Kwa kuwa Simba ndio inayoongoza ligi kwa kuwa na alama 78, ni sahihi kusema wanastahiki kutwaa ubingwa kwa mara ya tatu mfululizo. Wamefunga mabao 67 na kufungwa mabao16 tu. Wamepata sare mara tatu na kupoteza mechi tatu na kushinda mechi 24.

Ingawa husemwa kandanda ni mchezo wa bahati, lakini kwa jinsi nilivyowaona wachezaji wa Simba walipopambana na Mwadui, nilivutiwa kwa namna walivyomiliki lile gozi la ng'ombe na kupeana pasi zenye uhakika, tena kwa mbwembwe. Hongera!

Kwa nini nisiwasifu ilhali mimi (Yanga), na wao (Simba), hatuivi hata tukipikwa chungu kimoja?

Wahenga walisema: "Kweli ikidhihiri, uwongo hujitenga." Maana yake ukweli unapojulikana uwongo unajitenga. Twakumbushwa kwamba ukweli wa jambo fulani utokeapo, uongo unaolihusu hautambuliwi tena au hauna nafasi. Huweza kutumiwa kumnasihi anayejaribu kusema uongo wa waziwazi.

Mtu anapofanya jambo zuri ana haki ya kusifiwa na kupongezwa hata kama ni mpinzani wako. Usipomsifu au kumpongeza, wapo wengi watakaofanya hivyo na kukufanya wewe mwenye chuki kubaki ukikodoa.

Najua wenzangu wa Jangwani watanichukia ninapoeleza ukweli wangu kuhusu wapinzani wetu wa Msimbazi, lakini huo ndio ukweli wenyewe.

Wahenga walisema: "Kweli ndio fimbo ya kukamata" wakiwa na maana ya kweli ni silaha nzuri maishani. Methali hii yatukumbusha umuhimu wa kuusema ukweli hata kama kwa kufanya hivyo tutaishia kuchukiwa na wenzetu.

Hebu nitumie fursa hii kuwaambia wapinzani wetu (Simba) kuwa: "Angakaanga, tu chini ya gae." Maana yake hata akikaanga vitu fulani sisi (timu ya wananchi) tuko chini ya gae alitumialo. Tutaishia kujua tu. Huweza kutumiwa kuelezea kuwa hamna siri inayofichika milele.

Ni kweli kwamba "Anayepanda kilele, hupiga kelele." Maana yake mtu anayepanda hadi kileleni hupiga kelele kujitambulisha. Methali hii hutumiwa kumpigia mfano mtu aliyepata madaraka au cheo cha juu kisha akaanza kujivuna au kujishaua mbele za watu.

Nikumbushe tu kwamba Yanga inayojiita mabingwa wa kihistoria. Kwa nini? Kwa sababu ni timu pekee nchini kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu mara nyingi zaidi.

Hata hivyo, "Hakuna refu lisilo na ncha." Maana yake hakuna jambo lisilokuwa na mwisho. Methali hii hutumiwa kumliwaza na kumfariji mtu aliyefikwa na shida au jambo lolote zito kwamba avumilie kwa kuwa shida hiyo haitakuwepo milele. Je, ndiko inakoelekea Simba sasa? "Hatua ndefu hufupisha mwendo." Mtu atembeapo kwa hatua ndefu huikamilisha safari hata kama ni ndefu sana. Methali hii hutumiwa kumhimiza mtu anayefanya kazi ngumu na nzito kuwa ataishia kuimaliza, mradi aifanye hatua kwa hatua.

Kwa timu ya wananchi, methali ifuatayo iwatie nguvu: "Hauchi hauchi unakucha." Mtu husema usiku hauchi, hauchi, lakini hatimaye jua huchomoza na usiku ukatoweka.

Timu zote mbili zinazoitwa 'watani wa jadi' ilhali ni 'maadui wa jadi,' hebu zisome methali ifuatayo, labda zaweza kujisahihisha na kuwa waungwana, yaani watu wenye tabia njema.

"Hasama (uadui) ndimi za moto." Uadui au adawa ni kama ndimi za moto ambazo huchoma. Methali hii inatuhimiza tujiepushe na uadui unaoweza kutuletea maangamizo makubwa.

**TAFAKURI (Uwezo wa kuzingatia jambo).**

**marobarnabas@yahoo.com**

## HABARI KITAIFA

# Wakulima wauza ufuta shingo upande

**Na Stevie Chindiye,** TUNDURU

WAKATI kukiwa na taarifa za kuanguka kwa soko la ufuta katika soko la dunia,wakulima wilayani Tunduru wamekubali kuuza zao hilo kwa shingo upande kwa bei ya wastani wa Sh. 1,516 kwa kilo.

Kufuatia hali hiyo, wakulima hao wameendelea kuililia na kuiomba serikali kuangalia uwezekano wa kuingilia kati kwa kuwatafutia wanunuzi watakaotoa bei nzuri na kuwaletea wakulima hao, kutokana na kupanda kwa gharama za pembejeo.

Katika mnada uliofanyika kwenye ofisi za chama cha AMCOS, bei ya juu ilikuwa Sh. 1,622 na ya chini ni Sh. 1.450 kwa kilo.

Wakiongea kwa niaba wa wakulima wa zao hilo, Mbina Mnanka, Samkumu Mohammed, Isa Salumu, Issa Bakari na Selemani Mussa, walisema wameridhia kuuza ufuta huo baada ya kubaini wengi wa wanunuzi wanaojitokeza kununua mazao yao ni madalali ambao wamelenga kujinufaisha kupitia migongo ya wakulima.

Walisema pamoja na kuwapo kwa maelekezo kuwa serikali haijihusishi na biashara, wanaimani serikali itawasaidia kwa kuwa mnada uliopita ufuta wao uliuzwa kwa wastani wa Sh. 2,047.26 wiki moja baadaye bei ilishuka kwa wastani wa Sh. 400 na mnada wa saba bei ilishuka zaidi.

Walisema bei hizo siyo rafiki kwa mkulima na hazizingatii gharama zilizotumika wakati wa kuandaa shamba, kulima, kupalilia, kupulizia dawa na kuvuna.

"Bei zinazotolewa na madalali wa wanunuzi hao kwa kisingizio cha kushuka kwa soko la dunia kutokana na corona zinatukatisha tamaa wakulima kuendelea kulima zao hiloo ikilinganishwa na gharama tunazotumia kuhudumia mazao yetu," alisisitia salumu.

Wakulima hao walisema huenda madalali hao wanafanya hivyo kutokana kutokuwapo ushindani wa kampuni nyingine katika minada hiyo ambayo tangu ianze wanunuzi ni walewale.

Awali mwakilishi wa Meneja wa Chama kikuu cha Ushirika wa wakuliwa Wilaya ya Tunduru (TAMCU), Yasini Masiano, aliwataka wakulima walioshiriki katika mnada huo kuwa makini kusikiliza bei zinazosomwa kutoka kwenye barua za wanunuzi walioomba kununua mazao yao ili waweze kuchagua bei kubwa kuliko zote.




Mkuu wa Kitengo cha Masoko na Mawasiliano wa Benki ya Stanbic Tanzania, Desderia Mwegelo, akimkabidhi Mganga Mkuu wa Serikali, Prof. Abel Makubi, mfano wa hundi yenye thamani ya Sh. milioni 50 ambayo ni mchango wa benki hiyo kwa kazi zinazoendeshwa na Wizara ya Afya. Kulia ni Mkuu wa Idara ya Huduma za Biashara na Uwekezaji wa benki hiyo, Manzi Rwegasira. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mpina apiga marufuku operesheni haribu maziwa

**Na Frank Kaundula**

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina, amesitisha operesheni ya Bodi ya maziwa ya kuharibu maziwa ya wafanyabiashara kwa kuyawekea rangi na mafuta ya taa, baada ya kubaini ukiukwaji wa sheria na kuitaka Bodi hiyo kuandaa mikakati ya kuwasaidia kukidhi matakwa ya kisheria.

Waziri Mpina alifikia uamuzi huo juzi katika operesheni yake iliyoanza saa 10 alfajiri maeneo mbalimbali jijini Dar es Salam, akilenga kujionea uhalisia wa biashara hiyo, baada ya kufikiwa na taarifa za malalamiko ya wafanyabaishara wanaodai kutotendewa haki na maofisa kutoka Bodi hiyo.

Aliwataka watendaji waliopewa jukumu la kutoa huduma ikiwamo kuwaongoza wafanyabiashara, kuzingatia wajibu wao kwa kuwasaidia wafanyabiashara, badala ya kuwakatisha tamaa.

"Sasa ni marufuku kuja kufanya hizi ukaguzi za kuja kuweka rangi kwenye maziwa ya wananchi na kuweka mafuta ni marufuku, kazi yao kubwa wanayotakiwa kuja kufanya hapa ni kusisitiza ubora na namna ya kuwabadilisha ili mzalishe kwa tija," alisema Mpina.

Awali kabla ya uamuzi huo, wafanyabiashara hao walisema wanatambua hatua zinazochukuliwa na Bodi ni matakwa ya kisheria, changamoto ni namna ya kumudu gharama za vifaa vinavyohitajika, ikizingatiwa wengi wao ni wafanyabiashara wadogo.

Ester Elius, mmoja wa wafanyabiashara wa maziwa, alisema kutokana na operesheni hizo wamehabiriwa maziwa yao na kurudishwa nyuma.

"Mtaji wetu ni mdogo hatuna uwezo wa mtaji wa milioni tano, wengi tunatembeza lita kumi au ishirini ndio maana tunapata wakati mgumu kutumia hivyo vifaa ambavyo vinauzwa zaidi ya Sh. laki tano, tunaumia sana wanavyotuwekea rangi na mafuta ya taa kwenye maziwa," alisema Ester.

Bodi ya maziwa wakijibu malalamiko hayo, walisema kilichofanyika ni usimamizi wa sheria, wakisisitiza ni wajibu wao kulinda afya za walaji hatua za kuharibu baadhi ya bidhaa, ni msingi wa utekelezaji wa majukumu yao.

Hata hivyo, waziri Mpina aliruhusu wafanyabiashara hao kuendelea na utaratibu wa awali, wakati viongozi wa bodi wakijipanga kutafuta suluhu, kuwawezesha kumudu gharama za vifaa vinavyotakiwa kisheria.

# Wanawake watakiwa kuchangamkia ubaharia

**Na Gwamaka Alipipi**

WANAWAKE nchini wametakiwa kuchangamkia fursa ya kusoma fani ya ubaharia, kuondokana na fikra kwamba ni kazi ya wanaume.

Rai hiyo ilitolewa jana na Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC), Emmanuel Ndomba, wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu Siku ya Maadhimisho ya Mabaharia Duniani.

"Idadi ya mabaharia duniani ni milioni 1.6, nchini idadi ni 5,300, lakini kati ya idadi hiyo mabaharia wanawake ni asilimia moja tu, hivyo tuna uhaba mkubwa wa mabaharia wanawake nchini," alisema Ndomba.

Kuhusu athari zilizowapata mabaharia wakati wa mlipuko wa ugonjwa wa corona, Ndomba alisema mabaharia wengi duniani walikumbwa na changamoto mbalimbali ikiwamo meli kuzuiliwa kuingia katika baadhi ya bandari na kusababisha kukaa majini kwa muda mrefu.

Alisema athari nyingine ni mabaharia walikosa huduma muhimu kama matibabu na kutengwa, huduma za kiburudani kama sehemu za mapumziko washukapo bandarini, walishindwa kuungana na familia zao pamoja na kuchanganyika na jamii.

Alisema makatazo hayo yalisababisha meli kukosa huduma na mahitaji muhimu zipatikanazo bandarini ikiwa ni pamoja na chakula, maji, dawa.

"Kutokana na nchi nyingi kufunga mipaka yao, meli zilikuwa zinazuiliwa kupiga nanga katika nchi husika, hivyo walikuwa wakilazimika kukaa katika meli kwa muda mrefu, wengine walikatazwa kushuka kwa madai kwamba wataeneza ugonjwa wa corona," alisema Ndomba.

Ndomba alisema TASAC kwa kushirikiana na serikali wameweza kuhakikisha kazi za mabaharia na taaluma za kibaharia zinatambuliwa sasa kuliko wakati mwingine.

Naye Mwenyekiti wa Chama cha Wanawake wanaofanya kazi sekta ya bahari Afrika Mashariki na Kusini (Womesa), Fortunata Kakwaya, alisema sababu kubwa inayochangia wanawake wasijiunge na ubaharia ni kutojiamini.

Alisema sababu nyingine ni kutopata nafasi ya mafunzo ili wawe maofisa.

Naye Mkuu wa Chuo cha Ubaharia Dar es Salaam (DMI), Erick Massami, alisema wamejiandaa kukuza uchumi kupitia kuzalisha wataalamu wengi wenye ujuzi wa ubaharia.

Alisema DMI kimekuwa chuo bora cha kutoa wahitimu wenye sifa za ubaharia, ambao kwa sasa wamezagaa katika nchi mbalimbali wakifanya kazi.

Massami alisema nchi nyingi Afrika kama Malawi, Kenya, Uganda zinaitegemea DMI katika kuchukua wahitimu wa fani ya ubaharia.

# Serikali yaagiza miradi ardhi kupewa hati

**Elisante John,** SINGIDA

SERIKALI imezitaka halmashauri za wilaya, miji, manispaa na jiji nchini, zinazomiliki ardhi na vituo vya mabasi, kuwa na hati za ardhi kwaajili ya kuiongezea serikali mapato yanayotokana na tozo la kodi kwenye miradi hiyo.

Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, alisema hayo wakati akizindua ofisi ya ardhi ya mkoa wa Singida, kati ya mikoa 26 ya Tanzania bara ambayo serikali inatarajia kila mmoja kuwa na ofisi hizo.

Waziri Lukuvi alitoa agizo hilo kufuatia Manispaa ya Singida kukabidhiwa rasmi hati ya ardhi, baada ya ofisi ya ardhi mkoa huo kuipatia manispaa hiyo hati, kwa ajili ya mradi wake wa kituo cha mabasi cha Misuna.

Akihutubia wananchi, Waziri Lukuvi aliwaagiza wakuu wa wilaya wajitahidi kumaliza tatizo la mipaka baina ya kijiji na kijiji, ambayo iliwekwa kwa mfumo wa alama zas GN, bila kuathiri upande wowote na kwa maslahi binafsi.

Alisema utaratibu huo utaondoa migogoro kwa jamii, na hivyo kuiondolea serikali lawama kutoka kwa wananchi.

Katika hatua nyingine waziri Lukuvi alitoa siku 90 kwa wamiliki wa viwanja zaidi ya 37,000 kati ya 43,200 vilivyopimwa mkoani humo, kufanya malipo ili wapatiwe hati zao za ardhi.

Alifafanua kuwa, licha ya wamiliki wa viwanja hivyo kunufaika na hati hizo, hivi sasa wanaikosesha serikali mapato, kutokana na viwanja vyao kutolipiwa malipo yoyote.

Awali, akiongea kwa niaba ya Kamishina wa Ardhi Msaidizi mkoani hapo, Ruteganya Speratus, alisema ofisi yake tangu ifunguliwe Machi 3, mwaka huu, imepokea ramani 1,330 kutoka Dodoma, zenye viwanja 43,227, zikiwamo 78 zenye kuonyesha mipaka ya vijiji 30.



Wakazi wa Jiji la Dar es Salaam, wakipita jirani na taka zilizorundikwa kando ya barabara jirani na Shule ya Msingi Rutihinda, eneo la Kigogo, jijini humo jana. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE.**

# Mafia yapania kuondoa ziro kuweka wanafunzi kambini

**Na Futuna Seleman, MAFIA**

HALMASHAURI ya Wilaya ya Mafia, mkoani Pwani inahitaji Sh. milioni 119 kufanikisha mpango wa kuwawezesha wanafunzi kufundishwa wakiwa kambini katika shule mbili ya Kitomondo na Bweni.

Mpango huo unalenga kuondoa mtazamo hasi kwa baadhi ya wazazi kuwashawishi watoto wao wasifanye vizuri mitihani yao ya taifa.

Akizungumzia mpango huo, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mafia, Erick Mapunda, alisema zaidi ya wanafunzi 400 wa kidato ha nne watapiga kambi katika shule hizo.

"Kiwango hicho ni sehemu tu ya mahitaji yenu muhimu tumepata kianzio Sh. milioni 20, tunahitaji milioni 100 ili tuweze kufanikisha mpango huu kwa maana hiyo tunatoa wito kwa taasisi ya Kalamu inayosaidia jamii pamoja na kutusaidia vyakula na vifaa mbalimbali kama itapata fursa itusaidie zaidi na wadau wengine wajitokeze kitusaidia," alisema Mapunda.

Aliishukuru taasisi ya Kalamu kwa kutoa motisha kwa wanafunzi waliofaulu kwenda sekondari mwaka jana na kuokoa wanafunzi ambao wangeshindwa kwenda shuleni kwa kukosa vifaa zikiwamo sare za shule.

Kwa upande wake Mkuu wa Wilaya ya Mafia, Shaibu Nnunduma, alisema wadau wana fursa kubwa ya kumaliza hali ya Mafia kuwa ya mwisho kila mwaka.

"Tunaweza kuibadilisha hii hali tukawa wa kwanza na ndio maana tukaja na mpango ambao tunaweza kuufanyia kazi, tumekuja na mpango mzuri tunajua matatizo yetu yako wapi tufanye tunajua moja ya tatizo tulilonalo ni idadi ndogo ya walimu, tulifikiria tukiweka wanafunzi kwa pamoja tukiwatumia vizuri kwa kuwafundisha wanafunzi wetu itakuwa ni moja ya njia ya kuwatoa kuweza kufaulu," alisema.

"Kipindi cha miaka minne wanafunzi wakiwekwa pamoja wakaambukizana uzoefu maarifa tunaamini kabisa jambo hilo linaweza kubadilisha mtazamo wao wakafaulu."

Alisema kuna tatizo kwa baadhi ya wazazi kuwashawishi wanafunzi wasifanye vizuri kwenye mitihani yao na kwamba kuwaweka kambini kutamaliza changamoto hiyo na kuwasaidia wanafunzi kutimiza ndoto zao.

Alisema njia ya kuwaweka wanafunzi kambini itasaidia kupatikana viongozi wa ngazi za juu kwa siku za usoni.

Alisisitiza jambo hilo lisiangiliwe kwa mtazamo potofu wa uchaguzi mwaka huu, mambo mengine lazima yaendelee kwa kuwa mitihani haitasimishwa na shule zitafunguliwa Juni 29.

Aliwataka wazazi wawaruhusu wanafunzi kwenda kwenye kambi hizo kwa kuwa faida wataiona siku za usoni.

"Sitarajii kuwa na mzazi atakayeshika watoto mashati ili watoto wasisome, sitarajiii wale ambao wamepanga kuwavuta mashati wenye nia njema kutaka kuwachangia unamvuta shati asichangie....,"alisema mkuu huyo.

Tayari wadau wa maendeleo sekta ya elimu taasisi ya elimu ya Kalamu na taasisi ya kimataifa inayosaidia jamii ya NAMA zimeisaidia wilaya hiyo mahitaji mbalimbali kwa wanafunzi hao ikiwamo vyakula.

# Wakulima waomba elimu dhidi sumukuvu

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

WAKULIMA wa zao la mpunga mkoani hapa wameingiwa hofu baada ya kuwapo taarifa za vifo vinavyosababishwa na sumukuvu na kuiomba Wizara ya Kilimo kupitia Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) Dakawa, kutoa elimu.

Hatua hiyo inatokana na kuwapo kwa elimu duni inayotokana na uelewa mdogo wa sumukuvu, hatua inayo changia kuleta madhara kwa watumiaji wa vyakula vinavyotokana na kilimo cha nafaka.

Wakulima hao walitoa ombi hilo wakati wakipatiwa mafunzo kuhusu madhara ya sumukuvu na matumizi ya mbegu bora za kisasa yaliyotolewa na TARI Dakawa kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo.

Mmoja wa wakulima hao kutoka wilayani Mvomero, Halima Jumanne, alisema elimu kwa wakulima na wananchi itasaidia kupunguza madhara hayo.

Alisema hofu imejengeka kwa wakulima kutokana na kuwapo kwa taarifa kutoka mkoani Dodoma kuwa sumukuvu hiyo imesababisha vifo na hivyo baadhi ya wakulima kukosa soko katika mazao yao yakiwamo mpunga na mahindi.

Naye mkulima Schola Libangu, kutoka Wilaya ya Kilosa, alisema bado uelewa wa wakulima kuhusu kuzalisha sumukuvu ni mdogo hasa kwenye mazao ya nafaka na kuiomba serikali kupitia Wizara ya Kilimo kutembelea maeneo ya uzalishaji wa mazao hayo kutoa elimu hiyo ili kupunguza hofu.

"Wakati mwingine mkulima hujikuta anazalisha sumukuvu bila kujijua baada ya kuifadhi nafaka zake bila kufuata utaratibu wa uhifadhi, hili linapaswa kutolewa elimu ya mara kwa mara hasa kwa wanaolima nafaka katika maeneo ya vijiji," alisema Libangu.

Mkurugenzi Msaidizi wa Idara ya Usalama wa Chakula, Josephine Amollo, alisema wizara imeamua kuanza kutoa elimu ya ulewa wa sumukuvu baada ya kubaini wakulima wa wilayani Mvomero na Kilosa kutokuwa na mbinu za kuzuia uzalishaji wa sumukuvu kutokana na kukosa elimu hiyo.

Alisema lengo la mafunzo hayo ni kuhakikisha wakulima wa mazao hayo wanaongeza uzalishaji kwa kutumia mbegu za teknolojia ya kisasa ambazo kwa sasa zinahitajika kutumika kama malighafi kwenye uchumi wa viwanda.

Mtafiti kutoka TARI Dakawa, Phabiola Langa, alisema licha ya mafunzo hayo, wakulima wanajengewa uwezo na uelewa wa matumizi bora ya mbegu zilizofanyiwa utafiti wa kina wa kupambana na wadudu waharibifu na kuongeza uzalishaji hasa wa zao la mpunga.

# Askofu apinga kujua kusoma, kuandika kuwa kigezo ubunge

Na Paul Mabeja, DODOMA

ASKOFU wa Kanisa la Agape Sanctuary Church, Nkuhungu jijini Dodoma, Juvenal Kabunduguru, amesema ipo haja kwa Katiba kufanyiwa marekebisho katika kipengele cha sifa mojawapo ya wagombea ubunge iwe kujua kusoma na kuandika.

Askofu Kabunduguru, aliyasema hayo jana jijini hapa, wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanyika Oktoba, mwaka huu.

Alisema ili kupata wabunge wenye uwezo mzuri wa utendaji kazi, kipengele cha sifa hizo kifanyiwe marekebisho.

"Haiwezekani mhudumu wa ofisi au dereva lazima awe na sifa ya kidato cha nne au cheti cha taaluma, lakini mbunge ni kujua na kusoma na kuandika basi, haiwezekani mbunge ambaye ndiye mwakilishi wa wananchi na anakwenda kutafsiri sheria za nchi na miswada mbalimbali muhimu, bungeni lakini sifa yake ni kujua kusoma na kuandika basi,"alisema.

Akizungumzia maoni ya watu katika maeneo mbalimbali ya Rais Magufuli, kuongezewa vipindi vingine vya kuongoza, alisema huko ni kukosa busara na hekima kwa kuwa mihula ya kuongoza kwa marais, inatakiwa kubaki kama ilivyo kikatiba.

"Hivi sasa wanasema tumuongeze muda wa kuongoza nchi Rais Magufuli, kwasababu yeye ni mzuri na amefanya mambo makubwa sana, lakini sasa siku akichukua nchi mtu ambaye ni mbaya itatubidi kupunguza tena miaka ya kuongoza? Viongozi nawaomba waache mihemuko ya kisiasa," alisema Kabunduguru.

Kadhalika, alisema kitendo cha Rais Magufuli, kuwa mgombea pekee katika nafasi ya urais ndani ya chama chake, anaona ni sahihi kwa kuwa hata sera za chama zinaeleza kuwa kiongozi aliyeko madarakani, anapaswa kuongoza kwa vipindi viwili.

"Hivi sasa tumekuwa tukiona Zanzibar, ndiko kwenye mchuano mkali kutokana na wao hivi sasa Rais Shein, amemaliza mihula yake yote miwili na huku bara mwaka 2025, patakuwa hapatoshi CCM, kutawaka moto inaweza kuzidi hata ile ya 2015 kwa kujitokeza wagombea zaidi ya 40,"alisema.



Mkurungenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Chamwino, Athuman Masasi, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dodoma jana, kuhusu mabadiliko madogo ya matumizi ya ardhi katika baadhi ya maeneo ya Mji wa Chamwino Ikulu. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Kidato cha sita kuanza mtihani Jumatatu

Na Renatha Msungu, DODOMA

WATAHINIWA 1,321 wa kidato cha sita katika halmashauri ya Jiji la Dodoma, wanatarajia kufanya mtihani yao itakayoanza Jumatatu Juni 29, mwaka huu.

Hayo yalibainishwa jana na Ofisa Elimu Sekondari wa Halmashauri hiyo, Upendo Rweyemamu, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu maandalizi ya mtihani wa kumaliza kidato cha sita, mwaka huu.

Rweyemamu alisema kuwa maandalizi ya mtihani huo yamekamilika na vifaa vimewasili katika shule husika na kuwapo kwa vituo 12 vya kufanyia mtihani.

Alisema jiji hilo linatarajia kupata ufaulu mzuri kwa wanafunzi watakaofanya mtihani kutokana na kuandaliwa vizuri na kupata muda wa kufanya marudio kwa mada walizofundishwa.

"Wanafunzi wameandaliwa vizuri kitaaluma na kisaikolojia, nichukue nafasi hii kutoa wito kwa walimu wanaowafundisha wanafunzi wa bweni kuendelea kuwaandaa kisaikolojia na kwa wa kutwa, wazazi wachukue jukumu la kuwapa ushirikiano mzuri na kuwaandaa kisaikolojia kwa kuwa huu ni mtihani kama mitihani mingine," alisema Rweyemamu.

"Hali ya ufaulu itaongezeka kutokana na maandalizi yaliyofanyika, ukiangalia mada nyingi zilikuwa zimekamilika mapema kabla ya kuanza mapumziko ya corona."

**Wanafunzi wameandaliwa vizuri kitaaluma na kisaikolojia, nichukue nafasi hii kutoa wito kwa walimu wanaowafundisha wanafunzi wa bweni kuendelea kuwaandaa kisaikolojia na kwa wa kutwa, wazazi wachukue jukumu la kuwapa ushirikiano mzuri na kuwaandaa kisaikolojia kwa kuwa huu ni mtihani kama mitihani mingine**

# Gundi yatumika mbadala dawa za kulevya

Na Augusta Njoji, DODOMA

SERIKALI imesema licha ya kufanikiwa kudhibiti uingizaji wa dawa za kulevya kwa asilimia 90 kutoka nje ya nchi bado kuna tatizo la matumizi ya gundi na dawa tiba zenye asili ya kulevya.

Kufuatia hali hiyo, imesema imeweka mkakati maalum wa kudhibiti matumizi hayo.

Kauli hiyo ilitolewa jana jijini hapa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Jenista Mhagama, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu siku ya dawa za kulevya.

Alisema kwa mujibu wa taarifa ya mwaka 2019 ya Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Masuala ya Dawa za Kulevya na Uhalifu (UNODC), Tanzania imefanikiwa kupunguza uingizaji wa dawa za kulevya kwa asilimia 90 na mamlaka imeshinda kesi kubwa za wafanyabiashara wakubwa wa dawa hizo.

Hata hivyo, alisema kutokana na udhibiti huo, watumiaji wamejielekeza kwenye matumizi ya bangi, mirungi, gundi na dawa tiba hali iliyofanya serikali ijipange kupanua wigo wa kushughulikia na kudhibiti.

"Matumizi ya gundi ni eneo ambalo limewekewa mkakati maalum tumegundua watoto wanatumia, kimsingi tunaangalia uwezekano wa kuweka utaratibu ili matumizi ya gundi yadhibitiwe yasitumike kinyume, kama tunavyojua matumizi ya gundi yanatumika kwenye mambo mbalimbali, lakini wengine wanatumia kama kilevi,"alisema.

Alisema kuhusu dawa tiba wamejipanga kwa kushirikiana na Wizara ya Afya ili kudhibiti matumizi yake kama sheria ilivyoweka utaratibu wa wizara hiyo kusimamia dawa hizo.

Alisema kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia mwaka 2015 hadi Juni, 2020, jumla ya kilo za bangi 188,489.93, mirungi kilo 124,080.33, cocaine kilo 58.46 na kilo za heroin 635.57 zilikamatwa.

"Jumla ya watuhumiwa 73,920 walikamatwa, pia mamlaka imefanikiwa kufanya ukaguzi katika kampuni 167 zinazojihusisha na uingizaji wa kemikali bashirifu na kukamata kiasi cha lita za ujazo 480,000 na kilo 22,145 za kemikali bashirifu zilizoingia nchini bila ya kufuata utaratibu,"alisema.

Kadhalika, alisema maboresho ya Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na dawa za kulevya ambayo yalifanyika mwaka 2017 ambayo yameweka sheria kali zaidi kwa watakaojihusisha na biashara ya dawa za kulevya yamefanikisha mafanikio hayo.

"Pia tumefanikiwa kubaini na kuvunja mitandao mikubwa ya dawa za kulevya nchini ambapo mamlaka kwa kushirikiana na taasisi mbalimbali za kimataifa kama vile UNODC, Interpol, DEA, CIA na NCA imefanikiwa kwa kiasi kikubwa kudhoofisha na kuvunja mitandao mikubwa ya wafanyabiashara wanaojihusisha na biashara ya dawa za kulevya ndani na nje ya nchi,"alisema.

# WHO yaahidi ushirikiano afya ya wananchi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SHIRIKA la Afya Duniani (WHO), limeahidi kuendeleza ushirikiano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kuimarisha mifumo ya afya ya wananchi.

Mwakilishi mkazi wa Shirika hilo Zanzibar, Dk. Andemichael Ghirmy, alisema hayo wakati akikabidhi msaada wa vifaa kwa Wizara ya Afya vikiwamo vya kupambana na maradhi ya corona katika Ofisi ya Wizara ya Afya.

Dk. Ghirmy alisema WHO inathamini juhudi kubwa zinazochukuliwa na serikali kuwapatia wananchi huduma muhimu za afya na wanashawishika kuunga mkono juhudi hizo.

Aliipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kufanikiwa katika mapambano dhidi ya maradhi ya corona, na hali inaendelea vizuri, lakini amewataka wananchi kuendelea kuchukua tahadhari kwa kuwa nchi jirani bado ugonjwa huo upo na mizunguko ya watu inaendelea.

Akipokea msaada wa vifaa hivyo vyenye thamani ya Sh. 95,657,500.00, Mkurugenzi Mkuu wa Wizara ya Afya, Dk. Jamala Adam Taib, alilishukuru shirika hilo kwa misaada inayotoa katika sekta ya afya.

Alisema misaada hiyo imefanikisha mapambano ya maradhi ya mlipuko yanayotokea nchini na kusaidia kuwahudumia wagonjwa wa kawaida katika hospitali na vituo vya afya visiwani hapo.

Dk. Jamala aliwataka wananchi wasijisahau na waendelee kuchukua tahadhari na kufuata miongozo ya Wizara ya Afya kukabiliana na maradhi ya corona ingawa yamepungua kwa kiasi kikubwa Zanzibar.

# Zanzibar yatoa mwongozo, wanafunzi 40 kwa darasa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, imeutaka uongozi wa shule zote za maandalizi, msingi na sekondari kuhakikisha idadi ya wanafunzi darasani haizidi 40 ili kuwalinda watoto na ugonjwa wa corona.

Akizungumza na waandishi wa habari kuhusu utaratibu wa masomo baada ya shule kufunguliwa, Waziri wa wizara hiyo, Riziki Pembe, alisema shule ambazo zina wanafunzi wengi, watafuata utaratibu maalum wa shifti utaoelekezwa na wizara.

Waziri huyo aliitaka kila shule kuimarisha mazingira ya usafi ili kupambana na ugonjwa wa Covid-19 ikiwamo walimu, wanafunzi na wageni kunawa mikono na maji na sabuni, kuacha kusalimiana kwa kupeana mikono na kuvaa barakoa katika mazingira ya shule.

"Katika kipindi hiki, masomo yataendelea bila ya shule kufungwa mpaka wiki ya tatu ya mwezi Desemba 2020...Mapumziko yatakuwa kwa siku za sikukuu za kitaifa tu,"alisema.

Alisema uongozi wa shule unatakiwa kusimamia utekelezaji wa miongozo itakayoandaliwa na wizara ili kuhakikisha wanafunzi wanafuata maelekezo ya viongozi wao kujiepusha na maambukizi na hivyo kusoma kwa salama.

Aliwataka wanafunzi wajiepushe na mikusanyiko isiyo ya lazima wanapokuwa katika maeneo ya shule na nyumbani na kila mmoja awe mlinzi kwa mwenziwe.

Aliwataka wafanyabiashara katika maeneo ya shule kuzingatia kanuni zote za afya ili kuhakikisha huduma wanazozitoa kwa wanafunzi zipo salama.

"Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa kushirikiana na Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ na Wizara ya Afya, zitafuatilia kwa karibu shule zote ili kuhakikisha maagizo yote yaliyotolewa na serikali yanatekelezwa kikamilifu," alisema.

Waziri Pembe alisema wizara inapenda kusisitiza kwa uongozi wa shule zote, zihakikishe wanazingatia maagizo na maelekezo yote yaliyotolewa na Wizara ya Afya katika kujikinga na virusi vya corona.

Alisema pia walimu wanatakiwa kuongeza bidii katika ufundishaji na kukamilisha mihutasari ndani ya mwaka huu kufidia muda uliopotea shule zilipofungwa.

Kadhalika, wazazi na walezi wametakiwa kuhakikisha wanatoa ushirikiano wa karibu ili kuwawezesha watoto kusoma kwa usalama na kwa ufanisi mkubwa.



Mkurugenzi wa Jumuiya ya wanasheria wanawake Zanzibar, Jamila Mahmoud (kulia), akizungumza na wanafunzi wanawake wa vyuo vikuu mbalimbali, mjini Zanzibar jana, kuhusu masuala ya udhalilishaji wa kijinsia. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# TAMWA yahamasisha wanawake bidhaa karafuu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKURUGENZI wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA) upande wa Zanzibar, Dk. Mzuri Issa, amewataka wanawake wajasiriamali kisiwani Pemba kutumia vizuri neema ya zao la karafuu kisiwani humo kwa kuzalisha bidhaa mbalimbali.

Dk. Mzuri aliyasema hayo wakati akitoa taarifa kwa vyombo vya habari kuhusu bidhaa zinazozalishwa na wajasirimali hao kutoka Pemba.

Alisema zao la karafuu linaweza kuzalisha bidhaa mbalimbali ambazo zina soko kubwa ndani na je ya nchi iwapo wajasiriamali hao watazisanifu vyema karafuu hizo.

Akitolea mfano wa bidhaa zinazotokana na karafuu, alisema ni sabuni pamoja na liwa ambayo ni maalumu kwa ajili ya kusafishia mwili.

Aliwataka wajasiriamali hao kuanza kutangaza zaidi soko la kimataifa pia kuna uhitaji mkubwa wa bidhaa za asili kutoka Zanzibar hususani zinazoalishwa kwa kutumia karafuu.

Kwa upande wake Ofisa uwezeshaji wanawake TAMWA ofisi ya Pemba, Asha Mussa, alisema wanawake wengi kisiwa cha Pemba wamehamasika na kujiunga kwenye vikundi vya uzalishaji wa bidhaa.

Akitolea mfano, alisema pia wajasiriamali hao hawakuridhika na uzalishaji wa bidhaa hizo pekee pia wameanza kujiingiza katika ufugaji na tayari baadhi ya vikundi vinamiliki mabanda na wanaendelea na ufugaji wa kuku.

Akizungumzia kuhusu changamoto alisema ni ukosefu wa soko la uhakika kwa wajasiriamali na wakati mwingine wajasiriamali hao hulazimika kukaa na bidhaa zao ndani kwa muda mrefu.

Aliomba serikali na taasisi nyingine Zanzibar na nje ya Tanzania kujitokeza kwa wingi kuunga mkono jitihada za vikundi hivyo kwa kuwa kufanya hivyo kutawawezesha wanawake wengi kujikwamua kiuchumi na kuondokana na umasikini.

Akizungumzia kuhusu hali halisi ya uzalishaji wa bidhaa, mmoja wa wajasiriamali kutoka kisiwani Pemba, Sakina Ame Bakar, alisema wanajitahidi katika uzalishaji wa bidhaa bora na zenye viwango vya hali ya juu.

Alisema licha ya jitihada hizo, wanaendelea kukabiliwa na changamoto ya ukosefu wa soko bora na lenye uhakika ambalo lingewafanya kuwa wajasiriamali bora na wakimataifa.

Aliomba serikali kuendelea kuwatengenezea mazingira ya kuwakutanisha na kampuni kubwa pamoja na wajasiriamali wengine wa kimataifa ili waweze kutengeza masoko mapya.

Nipashe
MWANGA WA JAMII
BT
BURUDANI TELE



TID
UKURASA 12

JUMAMOSI JUNI 27, 2020



## NYUMA YA PAZIA

# Vanessa Mdee kuacha Bongo Fleva

SAKATA la mwanamuziki Vanessa Mdee, kutangaza kuacha muziki wa Bongo Fleva, limeibua maswali ambayo majibu yake bado hayajapatikana.

Licha ya Vanessa mwenyewe kujitokeza hadharani na kutoa sababu lukuki za yeye kuamua kuchukua uamuzi huo, bado baadhi ya mashabiki wanaona hana sababu za msingi za kufanya hivyo na kudai pengine kuna siri nyuma ya pazia.

Hata hivyo, katika ufafanuzi wake, Vanessa, amesema ameamua kujitoa katika muziki kutokana na kukabiliwa na changamoto nyingi, ikiwamo msongo wa mawazo, ulevi na ugomvi na mama yake ambaye siku zote anapinga kazi hiyo.

Katika video yake inayopatikana kwenye You Tube, mrembo huyo alikuwa karibu na mpenzi wake ambaye ni Mnigeria, Rotimi, wakati akijaribu kufafanua jambo hilo.

"Najua baadhi ya watu ambao hawajui nini kazi ya muziki, hawanielewi hiki ninachosema, lakini muziki sio sehemu ya kawaida ya mwanadamu, ni kitu ambacho kwa mtu wa kawaida hawezi kunielewa," alisema Vanessa katika video hiyo.

Vanessa amesema baadhi ya sababu ambazo zimemfanya kujiengua ni pamoja na kuhofia kupatwa na matatizo ya kiafya, baada ya mara nyingi kuwa na msongo wa mawazo, presha za mashabiki na wakati mwingine kufanya mambo yaliyo kinyume na maadili ili kukidhi soko la muziki.

"Unatumia muda mwingi na kupitia changamoto, kuliko kile unachokipata. Siku zinapozidi kwenda, utendaji wa kazi unapungua na inapelekea kufanya vitu ambavyo havieleweki na haviendani na wewe ulivyo ili kutafuta soko," amesema.

Pamoja na ufafanuzi huo, baadhi ya mashabiki wake ambao walimfuatilia, walionekana kutokubaliana na kile anachokisema, wakieleza kuna kitu nyuma yake anakificha ambacho kimemfanya kuchukua hatua hiyo.

"Haiwezekani kuchukua hatua hii baada ya kumpata Rotimi, hili tulijua tangu mwanzo na ndio maana watu walimtahadharisha," ameisema Shaban Saidi. Amesema baada tu ya kukutana na mwigizaji huyo wa Marekani, alitangaza kuchukua mapumziko jambo ambalo watu wengi walibashiri dalili mbaya kwa msanii huyo.

Hata hivyo, wengine walimpongeza na kumtaka kumrudia Mungu kwa kuimba muziki wa Injili na sio kuacha moja kwa moja.

BASI SAWA

## Calisah usimung’unye, sema ukweli

WATU wamepigwa na butwaa baada ya kuibuka kwa madai kwamba mwanamtindo Calisah, kashindwa kulipa pesa baada ya kukodi gari la kutembelea.

Kulingana na EATV, Calisah, alifikishwa kituo cha polisi cha Urafiki na kutolewa dhamana na msanii Amber Lulu, kutokana na kurudisha gari aina ya Vitz ambalo alilikodi likiwa ameliharibu, huku akishindwa kulipa pesa kwa mmiliki wake.

“Aliniomba nimkodishie gari kwa siku tatu, tukakubaliana kila siku ni elfu 50 yeye alinilipa elfu 60 tu baada ya laki na nusu, akalirudisha gari halina mafuta, ameigonga vioo vya pembeni “side mirror”, ameiua monitor bila ya kuniambia na akani-block kwenye simu, nikamshtaki polisi kwa kuniharibia vitu vyangu venye thamani ya laki mbili na 60” amesema mmiliki wa gari hilo  aitwaye Edger.

Hata hivyo, mwenyewe Calisah, amekana kuhusika na jambo hilo “Sio kweli Sijawahi kukamatwa na polisi tangu mwaka huu uanze hizo ni stori za kizushi puuzieni, na kuna vitu vingi sana vinatokea na mimi nafahamika sana” amesema.



## TID akumbuka enzi hizooo!

MWANAMUZIKI mkongwe wa Bongo Fleva, TID, amekumbuka miaka mingi ya nyuma kiasi ambacho anatamani miaka irudi nyuma ili akutane na mpenzi wake Irene Uwoya.

TID, anakumbuka hata katika wimbo ule ‘Nilikataa’ ambao alimshirikisha Q Chifu, mrembo huyo ndiye alipamba video yake, lakini yote imekuwa kama historia kwake.

“Kipindi kile Irene Uwoya ilikuwa ni kazi yangu, lakini si unajua tena kinyamwezi hadi kwenye video, nilikuwa nam-date alikuwa ni mpenzi wangu,  nilikuwa sio mtu wa kuonyesha kama natoka naye ilikuwa ni vitu binafsi, kipindi kile alikuwa wamoto kuna muda natamani ku-date naye tena” amesema TID.





## Stara Fashion Week yarudi kwa kasi

JUKWAA la maonyesho ya mavazi la Stara Fashion Week, linatarajiwa kufanyika Julai 24 hadi 25th kwenye ukumbi wa Makumbusho ya Sanaa ya Taifa jijini Dar es Salaam.


Kwa mujibu wa mtoa taarifa hiyo jukwaa  hilo linafanyika kwa mara ya sita mwaka huu na litajumuisha wabunifu zaidi ya 30 kutoka kila kona ya Tanzania.

Maonyesho ya mavazi yatanza saa 10 hadi 12 jioni na kusindikizwa na Tuzo na burudani za kila aina.

Kauli mbiu ya mwaka huu ni Ubunifu Wenye Tija, Eco Fashion. Lengo kuu likiwa ni kuhamasisha jamii kutunza mazingira na mavazi.

Wabunifu katika maonyesho hayo wamepitia semina elekezi ya namna ya kupunguza Taka (Reduce), kubadili matumizi (recycle) na kutumia upya (Reuse) na wako tayari kuwa mfano wa wabunifu wanaojali,  kulinda na kutunza mazingira.

Katika  jukwaa hilo pia kutakuwa na fursa ya biashara kutoka kwa wajasiriamali mbalimbali.



## Uke wenza wamchanganya Shilole

AMA kweli wivu hauna mwenyewe! Ndivyo mwanamuziki na mjasiriamali, Shilole, anavyoonyesha kwa vitendo, baada ya kusema kamwe haitatokea kukubali kukaa uke wenza.

Akizungumza na EATV, Shilole, amesema haitatokea mumewe Uchebe, kuongeza mke wa pili hata kama dini inaruhusu, endapo ataamua kufanya hivyo, basi ataomba talaka ili aendelee na mambo yake.

“Nina furaha ndani ya ndoa yangu, ninajiamini na sina mambo mengi ndiyo maana najivunia kuwa na mume wangu,  ni ngumu kuongezewa mke wa pili kwa kweli la sivyo aniache mimi aoe mwanamke mwingine, hata kama dini inaruhusu ila mimi sitakubali” amesema Shilole.

## Vipi ngoma hizi zingeimbwa na Zuchu, Nandy?



**Na Adam Fungamwango**

HIVI sasa kuna wimbi la wasanii wengi wa kike wakiongozwa na Nandy na Zuchu ambao wanabamba kinoma kwenye muziki wa kizazi kipya.

Hata hivyo, bado kuna tatizo la watoto wa kike kuendelea kuimba furaha za mapenzi tu, lakini wakisahau kuwakumbusha akinamama kuwa pamoja na yote hayo, bado kuna changamoto kubwa sana kwenye mapenzi na ndoa, hasa kwenye mfumo dume uliopo.

Siyo mbaya kuimba furaha kwenye ndoa, au mapenzi, lakini wakati mwingine tunaona kunakuwa na matatizo makubwa kwenye mapenzi kiasi cha kuleta mtafaruku, hivyo kukumbushana inakuwa ni wajibu.

Kuna wanawake wengi yamewakuta makubwa kwenye mapenzi, au kwenye maisha ya kawaida, hivyo wasanii wa kike, pamoja na kuimba mapenzi, lakini ni lazima waingie kwa undani zaidi na kuwakumbusha wanawake wenzao madhila yanayotokea wakati mwingine, ili wanapotaka kuingia wajiandae na kujitafakari na si kujiingiza kichwa kichwa.

Wanamuziki wa zamani, tena wanaume, walikuwa wakijivisha uhusika wa wanawake na nyimbo zao kupendwa mno na akinamama.

Hizi ni baadhi ya nyimbo hizo, ambazo zinatakiwa sasa maudhui yake kama haya kuimbwa na akina Nandy na Zuchu watakapoamua kufanya hivyo.

**Mtoto Nampenda-Juwata Jazz Band**

Ni wimbo wa Msondo Ngoma uliotungwa na marehemu Selemani Mbwembwe ambao maudhui yake ni kwamba mwanamke analalamika kuwa  mumewe amekuwa akimsema kwa watu kwamba anamaliza pesa zake bure lakini hazai. Mwanamama anamwambia mumewe kama ni mtoto hata yeye anampenda, lakini uwezo hana na hii yote ni kazi yake Mola. Mwisho anamwambia kama hamtaki, basi ni bora tu aende zake.

**Chiapo-Vijana Jazz Band**

Wimbo huu wa Vijana jazz, uliotungwa na Hamza Kalala,  unamuelezea mwanadada mmoja ambaye anamsuta bosi kwenye kampuni moja ambaye amekuwa akimzungusha kumpa kazi, ingawa zipo zimejaa tele. Kazi ofisini mwake zataka watu, lakini kumbe alikuwa akimtaka kimapenzi kwanza ndiyo ampe kazi, mwanamama amemshtukia na sasa anampasha.

**Wifi Zangu Mna Mambo-Vijana Jazz Band**

Ni utunzi wake marehemu Hemed Maneti. Lakini ukatendewa haki sana na mwanamama Kida Waziri. Maudhui ni kwamba mwanamke anawatemea nyongo mawifi laivu. Anawaeleza kuwa amechoshwa na vituko wanavyomfanyia kila kukicha. Anawaambia anavumilia, lakini iko siku atachoka na kuondoka, lakini shida itakuwa kwa kaka yao atakayebaki peke yake.

Anawachana kuwa hawajui nini kaka yao anachompendea, wao wamebaki na dhana tu kuwa ni limbwata.

**Stendi ya Basi-Tomatoma**

Kwenye wimbo huu uliotungwa na marehemu Adam Bakari, ni kwamba mke anamjibu mumewe kuwa hachelewi huko anakodhani yeye, ila ni stendi ya basi kwa sababu ya tabu ya mabasi.

Yalikuwa ni majibu baada ya mume kumwambia mkewe kuwa siku hizi amekuwa akichelewa kurudi nyumbani kutoka kazini.

Ikumbukwe kuwa zamani mabasi yalikuwa tabu, lakini kulikuwa hakuna foleni barabarani, lakini kwa sasa utetezi wa mke ungeweza kuwa anachelewa kwenye foleni, kwa sababu siku hizi hakuna tabu sana ya mabasi kama zamani.

Wivu-DDC Mlimani Park Orchestra

Mwanamke kwenye wimbo huu kamkalisha kitako mumewe na kuanza kumhoji kwa nini amezidisha wivu kupindukia? Na pia inaonekana kama vile hamuamini?

Anakwenda mbali zaidi na kumwambia amegundua hata kazini haishi kuaga na kurudi kumchunguza nyumbani.

Mume anajibu siyo wivu, ila anaona uchungu kusikia maneno kwa majirani kwa hiyo amekuwa na wasiwasi.

## Masumbuko: Sumu ya mke sawa ya nyoka

**Na Adam Fungamwango**

WAHENGA walisema pesa na mali haziwezi kuvunja undugu, bali mke anaweza kusambaratisha undugu.

Mwanamke akiwa mwema, basi familia inaweza kuungana na kuwa pamoja, lakini akiwa na matatizo kuna hatari ya kusambaratika na kila mmoja kuishi kivyake.

Hii ipo sana kwenye jamii yetu hasa za Kiafrika, watu bado wanaendelea kuishi kijamaa zaidi. Hata watunzi wa hadithi, riwaya na filamu wanalizingatia sana hili wanapofanya kazi yao hilo.

Ukweli kuhusu hili unapatikana kwenye filamu ya ‘Masumbuko’. Ni filamu inayoonyesha uhalisia wa kuwa mwanamke ni kiungo kikubwa sana kwenye familia anapokuwa anataka kuiunganisha, lakini anapogeuka upande wa pili ana uwezo mkubwa wa kuisambaratisha familia yote.

Imechezwa na wasanii chipukizi kina Masumbuko Aboubakar kama Masu, Baraka Shaaban kama BK, Asia Salum kama Beth, Durudhira Kamba kama Nadya, Aisha Khamis kama Sindura na wengineo wengi.

Masumbuko ni kijana fukara aliyeishi na mkewe Nadya. Kutokana na ufukara wake, mke anaamua kuwa na uhusiano na mwanaume mwingine kwa ajili ya kukidhi mahitaji yake.

Hilo linaleta tatizo kubwa kwenye familia ya mumewe. Katika kuhangaika sana anapata kazi na kwenda kumwambia mke. Mke naye anamwambia hawara yake kuwa mumewe amepata kazi.

Hali hiyo inamtisha hawara ambaye ni BK kuwa sasa mume anaweza kumdhibiti mkewe kwa sababu atakuwa na kipato, hivyo anakwenda kwa mganga wa kienyeji kumroga.

Masumbuko anaanguka muda mfupi baada ya kukubaliwa kazini.  Ugonjwa huo unamfanya anaanza kutokwa na funza mwilini. Anarudishwa kijijini kwa mama na dada yake. Mama yake anakwenda kwa mganga na kugundua tatizo. Masumbuko anatibiwa na kupona. Anarejea mjini.

Kule ofisini nafasi yake bado ipo, hivyo anaanza rasmi kazi.

BK, anafukuzwa kazi kutokana na ubadhirifu na hii inamfanya Nadya kuanza kuhangaika na kwenda kuomba msamaha kwa Masu. Waswahili wanasema kupenda upofu, Masu anamrudia mkewe.

Kazi inaanza upya… Yoyote aliyefikiria atajirekebisha alikosea. Betha na mama yake alikwenda mjini kumsalimia kaka yao Masumbuko ambaye kwa sasa amekuwa na maisha mazuri, lakini walichokutana nacho ni balaa. Kila mmoja alifukuzwa kama mbwa ndani ya nyumba na Nadya, huku Masu akiwa hana la kufanya.

Siku zinaenda, Masu anapata habari kuwa mama yake mzazi amefariki kijijini. Anakwenda na mkewe kuzika. Wanachokutana nacho huko ni kufukuzwa. Betha, dada wa Masu na baadhi ya wanakijiji walisimama kidete kuhakikisha hamziki mama yake na anatimuliwa yeye na mkewe warudi mjini.





# Dbanj azidisha joto mtandaoni

NYOTA wa muziki wa Nigeria, Dapo Oyebanjo, maarufu kama Dbanj, amezidisha joto mtandaoni, baada ya mashabiki wake kutaka kuelezwa ukweli kuhusu madai ya kubaka yanayomkabili.

Juni 24, mwaka huu, habari ziliibuka baada ya jamaa mmoja anayeitwa Babatayo, kudai mwanamuziki huyo alimbaka msichana mdogo ambaye ni rafiki yake mwaka 2015.

Hata hivyo, mashabiki walicharuka katika Twitter wakionyesha hasira zao kutokana na madai yanayomkabili Dbanj, wakisema haki ipatikane kwani wao wanaona hana hatia.



## Bieber sema kweli, ulimbaka Daniella?

MWANAMUZIKI wa Pop, Justin Bieber, amejitokeza na kukanusha madai ya unyanyasaji wa kijinsia yaliyotolewa dhidi yake na mwanamke mmoja,

Mwanamke huyo anayeitwa Daniella, alitoa madai hayo kupitia mtandao wa Twitter, aliandika ujumbe mzito akimtuhumu mwanamuziki huyo kumnyanyasa kingono mwaka 2014.

Daniella, alidai alikutana na Bieber wakati akihudhuria hafla huko Texas, baada ya kutambulishana yeye na marafiki zake, msanii huyo alishambuliwa kimapenzi bila ridhaa yake.

Bieber alimesema siku ambayo mwanamke huyo anadai kushambuliwa, yeye alikuwa na ratiba zake za muziki sehemu nyingine.

## Uchemba kwa hili, Mungu yupo nawe

MWIGIZAJI mkongwe wa Nollywood, Williams Uchemba, amemuasili mtoto wa miaka 18, na kuahidi kumsomesha chuo kikuu.

Wiki hii, msanii huyo alimtambulisha kijana huyo katika ukurasa wake wa Instagram, akisema mtoto wake huyo atakuwa na ndoto yenye mafanikio kupitia baba yake.

Kulingana na Uchemba, tayari amemfanyia manunuzi mbalimbali ikiwamo samani ya chumba chake pamoja na vitu vingine muhimu kwa ajili ya maisha yake.





## Duh! Masteson usimsingizie shetani

SHETANI bado anawaandama wasanii wa filamu wa Hollywood, baada ya mwigizaji maarufu Danny Masterson, kukabiliwa na tuhuma ya kuwabaka wanawake watatu.

Mwigizaji huyo ambaye amejipatia sifa kemkem kupitia filamu ya vichekesho ya 'That 70s Show', amefunguliwa kesi katika majimbo matatu tofauti nchini humo, akishtakiwa kuwabaka kwa nguvu wanawake hao.

Kulingana na mtandao wa PageSix, Masterson ameshtakiwa kumbaka mwanamke mwenye umri wa miaka 23, mwaka 2001. Pia kesi nyingine anatuhumiwa kumbaka mwanamke mwenye umri wa miaka 28, Aprili mwaka 2003 na mwingine wa 23 ndani ya mwaka huo.

## Dan Foster aliliwa kila kona Nigeria

MASHABIKI wa filamu za Nollywood, wanaendelea kuomboleza kifo cha mkongwe wa uigizaji Dan Foster, baada ya kufariki dunia kutokana na ugonjwa wa Covid 19.

Foster alifariki dunia siku ya Jumanne ya wiki hii jijini Lagos na kuthibitishwa na mke wake Lovina.

Msanii huyo pia ambaye ni mtangazaji wa redio, anayejulikana kama 'The Big Dawg,' amejipatia umaarufu kutokana na kufanya vizuri katika utangazaji na baadhi ya filamu alizoshiriki.



## WAKATI SHULE ZINAFUNGULIWA...

# Wadau waorodhesha majibu kwa elimu iliyobomolewa na corona

## Waibua mbadala wa 'kila kitu darasani'

Na Mwandishi Wetu

SEKTA Elimu nchini sasa imepitia wakati mgumu, kuhusiana na maradhi ya corona yanayosababishwa na virusi vya Covid 19, ikiwa takriban miezi mitatu nchini wanafunzi wamekaa majumbani.

Ni sintofahamu ya mustakabali wao kimasomo. Hatimaye serikali imetangaza kufunguliwa keshokutwa, nchi nyingi zinazoendelea kama Tanzania, kuangukia changamoto, ikilinganishwa na kulikoendelea.

Ripoti ya Shirika la Umoja wa Mataifa ya Elimu na Sayansi (UNESCO), inasema maambukizi ya virusi Covid 19 yameathiri utoaji elimu kimataifa.

Kuna wastani wa watu bilioni 1.54, kati yao mabinti 743 hawapo shuleni na wanaangukia hatari ya kukosa fursa rasmi za elimu, hasa Afrika.

Mfano hai, unatajwa Kusini mwa Jangwa Sahara, hata kabla ya shule kufungwa takribani mtoto mmoja kati ya watano (asilimia 20) wenye umri kati ya miaka sita hadi 11, hawakuwepo shuleni.

Pia asilimia 20 za wenye miaka 12 hadi 14, nao hawapo masomoni kipindi hicho, hali kadhalika asilimia 60 kwa wenye umri kati ya miaka 15 na 17 wanaotakiwa shule za sekondari, hawapo.

Ripoti ya Shirika la Maendeleo ya Watoto Duniani (UNCEF) nchini inadokeza zaidi ya watoto milioni mbili wa shule ya msingi na milioni moja na nusu wa umri wa sekondari, hawapo masomoni.

**MTOTO/ SIKU YAKE**

Wakati kunaadhimishwa Siku ya Mtoto wa Afrika, Juni 16 kila mwaka, jamii inapaswa kutafakari changamoto zinazowakuta watoto.

Shirika lisilo la kiserikali la HakiElimu, liliandaa mdahalo kwa njia mtandao , kukutanisha wadau muhimu, tafakarisha na kujadili, pia kupendekeza namna bora ya kuzirahisisha changamoto za elimu nchini kuiwafikishia watoto elimu bora yenye usawa.

Mkurugenzi wa HakiElimu, Dk. John Kalage, anasema umuhimu wa watoto kujifunza shuleni uko wazi na cha kujifunza ni athari katika mifumo rasmi kujifunza.

Anasema hadi sasa wastani wa wanafunzi milioni 12 waliopo majumbani kwa miezi mitatu nchini.

**UPUNGUFU**

Dk. Kalage anasema katika kipindi shule zilifungwa nje ya kalenda rasmi, HakiElimu imegundua upungufu katika utoaji elimu kitaifa, akitaja maeneo ya kujifunza na kufundishaji, wanavyojifungia kwa kiasi kikubwa madarasani.

"Mijadala iliyoibuka kuhusu njia mbadala za kuendelea kujifunza na kumlinda mtoto wakati wa kipindi hiki cha COVID-19, ni ushahidi tosha namna ambavyo mfumo wetu wa utoaji elimu ulivyo nyuma ya wakati," anasema.

Mkurugenzi huyo, anatoa mfano njia mbadala ya kutumiwa televisheni na radio za kumuendeleza mwanafunzi kujifunza akiwa nyumbani ni mtihani.

Dk. Kalage anarejea ripoti ya utafiti wa Bajeti za Kaya, ikiwamo ya za makazi mwaka 2017-2018, nyumba zenye mawasiliano ya televisheni ni asilimia ya 43, simu (24%) na televisheni (78%).

Anasema, japokuwa wasikilizaji wa radio nchini na televisheni kupitia simu inaongezeka, changamoto inabaki sio kaya zote zinamudu matumizi, akimaanisha kundi la wanaotoka kwenye familia maskini.



Mwalimu na wanafunzi wake darasani. **PICHA: MTANDAO.**

Mapendekezo ya teknolojia ya kimtandao, anayapa upungufu kwamba, mbali na ujuzi mdogo walio nayo wazazi, walimu na wanafunzi, bado idadi kubwa ya wanajamii hawana uwezo kununua vifaa hivyo, hata kugharamia uendeshaji wake.

Anatoa mfano wa Ripoti ya Mamlaka ya Udhibiti wa Mawasiliano Tanzania (TCRA), Desemba mwaka jana, Tanzania ilikuwa na watumia mtandao 25,794,560.

Dk. Kalage anataja gharama za intaneti iko juu, mfano wa wastani 'MB 75' ni Sh. 1,000, kwa maana hiyo kuna bajeti ya shilingi 30,000 kwa mwezi.

Anasema ni familia chache na hasa masikini hazimudu gharama za mfumo huo wa elimu mtandao, hata wanaiweka kando.

Mkuu huyo wa HakiElimu, anasema ni bahati mbaya utamaduni wa elimu nchini, haumfanyi mzazi au mlezi kuwa sehemu kuu ya kujifunza kwa mtoto wake na mara chache kukuta walimu katika baadhi ya shule, wanatoa za ziada kwa mwanafunzi kuzifanya nyumbani.

"Hii inasababisha hatari zaidi kwa mwanafunzi kuwa nyumbani kwa kuwa anakosa uhakika wa kuendelea kujifunza kupitia wazazi au walezi," anasema.

Kalage anasema taarifa za UNICEF mwaka 2011, zinaonyesha matukio ya unyanyasaji watoto masomoni, yanatolewa njiani ama kwenda au kurudi shule.

Dk. Kalage anatoa mfano, taarifa ya mwaka jana ya Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), inaonyesha matukio hayo majumbani.

LHRC inarejea mwaka 2018/19 kulikuwapo kesi nyingi za wasichana kupata mimba; ubakaji na ulawiti yaliyoripotiwa polisi, ikisema kati ya Januari na Juni mwaka jana, kutoka majumbani na mitaani.

**USHAURI**

Anasema katika kipindi cha corona, serikali na wadau wengine wamejadili upatikanaji elimu na wakapata mipango chanya ya kuinua elimu, kupitia mbinu mbadala inayofaa kuwa fursa ya kujifunza namna bora ya kuimarisha mfumo wa elimu nchini.

Dk. Kalage anashauri janga corona ichukuliwe kama fursa ya mabadiliko na namna ya kuwekeza uendeshaji shule na taasisi za elimu nchini.

Anahimza umuhimu wa miundombinu na teknolojia ya mawasiliano ya habari (Tehama), akisisitiza uzoefu wa corona iwe fursa ya marekebisho ya sheria kama kodi, tozo na uwezeshaji wananchi na tekinolojia, uikiwamo kwa wazazi, walezi na walimu.

"Janga hili pia liwe fursa ya kuwafikia watoto ambao hapo mwanzo hawakuwa shuleni. Tumeona njia mbadala zikipendekezwa za wanafunzi kujifunza katika kipindi cha COVID-19," anasema Dk. Kalage.

Anakumbusha matukio ya ukatili kwa mtoto kama, ikiwamo kupata idadi kamili ya ujauzito, wazazi na wanajamii watafakari kwa kina namna ya kulinda watoto wa kike.

Dr. Kalage anaendelea: "Ningependekeza utafiti huu ufanyike kwa haraka ili kubaini idadi ya wasichana waliopata ujauzito na hivyo kuweza kuwasaidia kielimu."

**DK. MACHUMU WA DUCE**

Mtaaluma, Dk. Maregesi Machumu, kutoka Chuo cha Elimu cha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (DUCE), anawataka wadau elimu nchini kusimama kukabili ukatili na kuhakikisha ulinzi, usalama na haki za watoto.

Dk. Machumu anasema haki ya mtoto na kukemea maovu dhidi yao inaanza katika familia, akirejea kipindi cha corona matukio mengi yamefanyika, ikiwamo ndani ya familia au jirani, lakini wanabaki kimya kuhofu ugombanishaji au kuvunja uhusiano.

Anasema, pia corona imewaathiri wanafunzi kielimu, akitaja maeneo ya lishe na afya, kwani kabla shuleni walihudumiwa kiafya hata kuhudhuria kliniki.

Mtaaluma huyo anaomba uwezekano wa wadau wa elimu, wahusike kutafiti kwa kuwauliza watoto jinsi walivyofanyiwa ukatili, hali inayosaidia kujua uhalisia na kujenga picha halisi ya unyanyasaji watoto.

Mchangiaji hoja, Eliamani Laltaita, anasema corona limeathiri elimu kwa kiasi kikubwa, hivyo anashauri kuangaliwe njia nzuri itakayowasaidia watoto kukabili upungufu wa kukosa shule miezi mitatu.

Mjumbe wa Bodi ya HakiElimu, Mwalimu Richard Mabala, anasema kuna tatizo la muda mrefu katika shida ya elimu na corona imezidisha. Rai yake kasoro zizizopo kutatuliwa, ikiwamo kuacha kutumia Kiswahili katika masomo yanayofunzwa kwa Kiingereza.

Anasisitiza suluhisho la kimtaala, wanafunzi wafundishwa kwa lugha wanayoimudu.

- **Makala hii ni kwa mujibu wa mjadala wa kitaaluma kuhusu sekta elimu, uliondaliwa na asasi ya Haki Elimu.**

## KUELEKEA UCHAGUZI MKUU...

# Uwepo uhuru wa kutoa maoni, miiko izingatiwe

**Na Mwandishi Wetu**

UCHAGUZI wa viongozi kwa utaratibu unaokubalika kupitia sanduku la kura katika mazingira yaliyo huru na haki, ni moja ya nguzo muhimu za demokrasia. Hilo ndilo Watanzania wanalokwenda kulifanya Oktoba mwaka huu.

Nguzo nyingine muhimu ni ushirikishwaji wa watu, kuheshimu haki za binadamu na utawala wa kisheria unaozingatia na kuheshimu katiba.

Wakati Watanzania wanajiandaa kuchagua viongozi wa kiasiasa kuanzia madiwani, wabunge na rais, kinachohitajika na kila mmoja ni kuona kuwa Tanzania inakuwa na uongozi bora katika ngazi zote. Viongozi wanaowajibika, wenye uzalendo na nia ya dhati ya kuondoa umaskini unaowakabili wapigakura.

Dhana ya uongozi bora imejikita katika mchakato unaohusisha mwingiliano na ushirikiano baina ya watu, matumizi bora ya rasilimali, taasisi kufanya kazi pamoja, kufuata taratibu, tamaduni na kuweka mikakati mbalimbali ya kusaidia mamlaka halali iliyochaguliwa kidemokrasia kuongoza wananchi na kupata matokeo au kufikia malengo yaliyokusudiwa.

Kwa muktadha huo, katika uongozi wa kidemokrasia, uongozi bora ni lazima uwe shirikishi na unazingatia maoni ya wengi na hivyo kuendeleza uhuru wa kutoa maoni na haki ya kujieleza.

Ndiyo maana katika kuelekea uchaguzi mkuu wananchi wanao wajibu wa kutumia haki ya kikatiba ya kutoa maoni yao, kukosoa, kushauri na kupendekeza kwa viongozi kile wanachotaka kifanyike na kuwe na matokeo chanya.

Wananchi au wapigakura wanatakiwa kufanya nini, ili kutoa maoni yao na kutumia haki ya uhuru wa kujieleza kwa viongozi, watiania na wagombea wakati huu wa kuelekea Uchaguzi Mkuu?

Anna Henga, (pichani) ni Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu, katika mazungumzo na Nipashe, anabainisha wajibu wa wananchi na wanachotakiwa kufanya kuwafikia viongozi wao kupitia uhuru wa kutoa maoni na kujieleza.

**SWALI: Unafikiri wananchi wakati huu wa uchaguzi mkuu iwe kwenye kampeni au mikutano wanawezaje kutumia haki hii ya katiba ya uhuru wa kujieleza na kutoa maoni bila kuwa na misuguano?**

**HENGA:** Wanaweza kutoa maoni yao bila kutumia lugha za kuudhi kama matusi, wanaweza kuongea mambo yasiyodhalilisha utu au haki za wengine, mfano kudhalilisha wengine kijinsia na kuzungumzia masuala ya faragha.

**SWALI: Wakati huu wa uchaguzi wapigakura wanaweza kutumia mbinu gani kutoa maoni yao na uhuru wa kujieleza?**

**HENGA:** Mambo yako mengi lakini ni pamoja na jukumu la kuangalia ahadi za wakati wa kampeni zilizopita. Zipo ahadi zilizokuwa zinawavutia wananchi na kuelekea kuwa majibu ya shida zao, wanaweza kuchunguza je, matatizo yalitatuliwa kupitia ahadi hizo?

Ni wazi kuwa wapigakura wanakipigia chama kura kutokana na sera, miongozo na ahadi zake zinazotolewa kwenye kampeni wanapoona kuwa zitabadili maisha yao. Je, hayo yamefanyika? Ni jukumu lao kuhoji na kujadili.

Lakini pia ni wakati wa kutumia haki ya kutoa maoni na uhuru wa kujieleza kuuliza na kuhoji kuhusu ahadi hizo licha ya kwamba pengine haziko kisheria (not binding).

Vilevile, huu ndiyo muda wa kuchunguza ilani na ahadi zilizotolewa wakati wa uchaguzi na mpya zinazoelezwa katika uchaguzi ujao.

Jambo lingine ni kushiriki kuuliza maswali wagombea na watiania wakati wa kampeni. Ni muda pia wa kuandika barua kwa mamlaka mbalimbali zinazohusika na masuala ya uchaguzi, kutoa ya moyoni iwe mapendekezo, maboresho au ushauri kwa wahusika.

Wapigakura pia wanaweza kutoa mawazo kwenye vyombo vya habari, mitandao ya kijamii na mikutano ya serikali za mitaa kwa kuzingatia haki za binadamu na kufuata sheria na taratibu zilizoko.

**SWALI: Uhuru wa vyombo vya habari ni muhimu wakati huu wa uchaguzi. Hili nalo unalizungumziaje kwa kurejea ibara 18 ya katiba ya Jamhuri ya Muungani wa Tanzania pamoja na Sheria ya Huduma ya Habari ya Mwaka 2016?**

**HENGA:** Ibara ya 18 ya katiba iko vizuri kuhusu uhuru wa kujieleza na kupata habari. Tukiifuata kama ilivyo tutakuwa na uchaguzi huru na wa haki, unaokwenda kwa misingi ya kikatiba kwenye kulinda na kutetea uhuru wa maoni.

Sheria ya Haki ya Kupata Taarifa na ya Huduma za Habari tulishasema tangu awali kwamba zina upungufu ambao Mahakama ya Afrika Mashariki imeamuru Tanzania kuyarekebisha.

Uhuru wa vyombo vya habari ni muhimu katika kutoa taarifa za uchaguzi zinazolenga kueleza ukweli na kusimamia maadili. Kuwaeleza wapigakura habari zenye ukweli na zinazofuata taratibu za kisheria katika kuzikusanya na kuzihariri ili zitumike kuwaeleza wananchi na wapigakura masuala mazima ya uchaguzi kama sheria, kanuni na taratibu lakini na adhabu zinazotolewa iwapo watu watazikiuka.

Ni jukumu la vyombo vya habari iwapo kuna sintofahamu, kutafuta ukweli na kuwaelezea wananchi.

SWALI: Baadhi ya watu wanaamini kuwa matumizi ya intaneti yanaweza kuwa nguvu mpya ya kuongeza uhuru wa kutoa maoni pamoja na uhuru wa kupata habari wakati wa uchaguzi mkuu. Ni kwa vipi suala hili linaweza kufanikiwa au kukwama nchini?

HENGA: Mitandao ya kijamii ni njia mojawapo ya uhuru wa kutoa maoni. Ni muhimu watu wakaachwa huru kutoa maoni hayo maadamu hawadhalilishi utu wa mtu, kuvunja sheria na kuongeza migogoro




Kupiga kura ni haki yako ya msingi lakini pia kuzungumzia mafanikio, kuhoji upungufu, changamoto , ahadi zilizotolewa na udhaifu wowote wa kiongozi wako au serikali ni haki yako pia. **PICHA MTANDAO.**



# Kiongozi wa upinzani Malawi aongoza

**ILONGWE, Malawi**

KIONGOZI wa upinzani nchini Malawi, Lazarus Chakwera, anaelekea kupata ushindi katika kura ya uchaguzi wa marudio za urais baada ya matokeo yake kufutwa kufuatia madai ya udanganyifu.

Matokeo rasmi ya uchaguzi huo uliofanyika Jumanne hayajatangazwa na Tume ya Uchaguzi ya Malawi, lakini chombo cha habari cha serikali MBC, kilisema kiongozi huyo wa upinzani anaongoza na asilimia 59 ya kura zilizohesabiwa.

Chombo hicho kilieleza kuwa, Rais Peter Mutharika, ambaye anawania muhula wa pili, ana asilimia 38 ya kura zilizohesabiwa.

Kadhalika, mgombea wa tatu ambaye hakuonekana kama mgombea mkuu, Peter Kuwani, alipata asilimia mbili ya kura zote.

Mwaka jana, Malawi ilikuwa nchi ya pili barani Afrika kufuta matokeo ya uchaguzi wa urais kufuatia madai ya udanganyifu, baada ya nchi ya Kenya kufuta matokeo ya uchaguzi mkuu mwaka 2017.

Wafuasi wa Chakwera, walianza kusherehekea kile wanachoamini ni ushindi wa kihistoria kwa kuamini kuwa uchaguzi uliofutwa ulikuwa umegubikwa na udanganyifu. "Maisha mapya kwa Malawi," alisema kiongozi wa upinzani nchini Zimbabwe, Nelson Chamisa.

"Mungu ameipatia Malawi mcha Mungu," alisema akitaja historia ya Chakwera kama kiongozi wa dini.

"Ndugu yangu, rafiki yangu na kiongozi ameshinda uchaguzi wa Malawi. Niliwasiliana naye kwa simu na kusherehekea ushindi wake," alituma ujumbe wa twitter kiongozi wa zamani wa chama cha upinzani cha DA Mmusi Maimane.

*BBC*



Safari ya mwisho ya aliyekuwa Rais wa Burundi Pierre Nkurunziza.

# Maelfu wananchi burundi Wamzika Rais Nkurunziza

**BUJUMBURA, Burundi**

MAELFU ya wananchi wa Burundi wamejitokeza katika mji wa Gitega kuuaga mwili wa aliyekuwa Rais wa nchi hiyo, Pierre Nkurunziza, wakati ukielekea kuzikwa jana baada ya kufariki dunia mapema mwezi huu.

Nkurunziza, ambaye aliongoza nchi hiyo kwa miaka 15, alifariki dunia akiwa na miaka 55 kwa ugonjwa wa moyo.

Nkurunziza alizikwa katika mnara uliojengwa hivi karibuni huko Gitega katika eneo lililotengwa kwa ajili ya waathirika wa majanga mengine kwa miaka mingi, ingawa halikuwahi kuzinduliwa rasmi.

Jana ilitangazwa kuwa ni sikukuu ya taifa kwa ajili ya mazishi ya Nkurunziza.

Wanafunzi wa shule mbalimbali waliovaa sare zao na raia walijitokeza barabarani kusubiri msafara uliobeba mwili wake, kupita.

Uwanja wa Gitega ambapo hafla ya mazishi ilifanyika pia kulijaa raia kutoka kila pembe ya nchi hiyo, wote wakiwa wamevaa nguo za rangi nyeupe kulingana na ombi la serikali.

*BBC*

## Marekani yatuma Dola bil 1.4 za Corona kimakosa

**WOSHINGTON, Marekani**

WIZARA ya Fedha nchini Marekani, imetuma zaidi ya Dola bilioni 1.4 kimakosa ambazo ni sehemu ya fedha za kukabiliana na janga la corona kwa watu waliokufa.

Utafiti uliofanywa na Wakaguzi wa serikali wamebaini kuwa suala hilo ni moja ya changamoto zilizobainika katika mapitio rasmi ya msaada unaotolewa na Serikali kwa sababu ya janga la virusi vya corona.

Tangu Machi, Bunge limeidhinisha Dola trilioni 2.6 katika uchumi wa Marekani kama juhudi za kusaidia kukabiliana na mdororo kutokana na usambaaji wa virusi vya corona.

Wakaguzi hao walibaini kuwa, uharaka ya kutoa fedha hizo ulichangia kufanyika kwa makosa hayo.

Kadhalika, ripoti ya Ofisi ya Uwajibikaji ya Serikali ilibaini kwamba Wizara ya Fedha ya Marekani ambayo inasimamia utoaji wa hundi kwa familia za Marekani, haikuangalia rekodi za waliokufa, ingawa baadhi ya maofisa wa kodi wanaofanyia kazi mpango huo walizungumzia wasiwasi wao kuhusu hatari ya kutokea kwa makosa kwenye utumaji wa barua pepe.

Ripoti hiyo pia imeonya kwamba mpango wa kutoa mkopo kwa biashara ndogondogo ambao ni asilimia 26 ya pesa zilizotengwa kukabiliana na janga la corona, ulikuwa katika hatari kubwa ya kuingiliwa na walaghai, huku Utawala wa Biashara Ndogondogo ukitupiwa lawama kwa kukosa kutoa ushirikiano katika utoaji wa taarifa kuhusu mikopo na mipango yake ya usimamizi.

"Kwasababu ya idadi ya mikopo iliyoidhinishwa, kasi ambayo mikopo hiyo ilipitishwa na ukosefu wa usalama wa kutosha, kuna hatari kubwa baadhi ya programu za walanguzi ziliidhinishwa," wakaguzi wa serikali walisema.

Pia idara hiyo iliongeza kwamba kuna umuhimu wa kufanyika kwa mabadiliko ya kukabiliana na hatari kama hizo zinazoweza kutokea.

*BBC*

# Meli ya mafuta iliyokwama Bahari ya Sham yazua hofu

**SANAA, Yemen**

UMOJA wa Mataifa umesema kuwa meli ya kusafirisha mafuta iliyoachwa katika Pwani ya Yemen ikiwa na zaidi ya mapipa milioni moja ya mafuta ambayo hayajasafishwa iko katika hatari ya kupasuka au kulipuka.

Meli hiyo inaweza kusababisha uharibifu mkubwa wa mazingira kwa viumbe vya baharini katika bahari ya Shamu, viwanda vya kusafisha maji na njia za usafirishaji za kimataifa.

Wakati huo huo, waasi wa Kihouthi wanaodhibiti eneo iliko meli hiyo wamewakataza wakaguzi wa Umoja wa Mataifa kuingia katika meli hiyo.

Kwa mujibu wa Shirika la Habari la Associated Press, maji ya bahari yameingia katika sehemu ya injini ya meli hiyo ambayo haijawahi kushughulikiwa kwa zaidi ya miaka mitano na kusababisha kuharibika mabomba yake na kuongeza hatari ya kuzama.

*DW*

# HADITHI

# Mauaji Harusini-18

ILISEMWA hapo zamani kuwa dunia inaharibiwa na vitu viwili tu. Mapenzi na mali. Vitu hivi vinaweza kumfanya binadamu aende popote. Afanye chochote kile ili awe navyo, wengine wanakwenda mbali zaidi mpaka kutoa uhai wa wenzao.
Shani, binti wa kitajiri anapitia kwenye mikasa mikubwa mizito ya kupotezwa kwa wazazi wake na kumsababishia ukiwa na mawazo tele.
Wakati ikionekana binti huyo pekee kwa wazazi wake akielekea kurithi utajiri wa wazazi wake, kiu ya damu inaanza kuwaingia baadhi ya ndugu za wazazi wake ili apoteze maisha, wao waweze kumiliki mali hizo.
Hapo ndipo uhai wa Shani unapokuwa matatani na patashika nguo kuchanika inapoanza. Fuatilia mkasa huu kuburudisha, kuelimisha na kusikitisha.

**Na Adam Fungamwango, (0716 350534)**

"Hivi humu kweli unalala peke yako kweli?" Eddy aliuliza kimzaha.

"Ulitaka nilale na nani?"

"Mmmmh, nauliza tu, maana binti nzuri kama wewe kuwa huna mwenyewe kweli?"

"Sina mtu yoyote Eddy. Siyo kama watu hawagongani. Yaani ni balaa. Matajiri rafiki za baba, vijana wao, mamaneja wa kampuni, mawaziri, wabunge, wameshatupa ndoana we, lakini mimi nimewatolea nje."

"Kwa nini mtoto mzuri kama wewe unawatolea nje na unaishi peke yako, bila hata mtu wa kukuliwaza?"

"Kwanza umri wangu bado mdogo miaka 23 kwa hiyo sina papara sana. Muda upo. Nataka nitafakari kwanza kwa kina. Ninampata nani na ananitaka kwa nini?"

"Na mimi binamu yako pia hunitaki?" Eddy alimuuliza kwa mara nyingine kwa utani.

Shani aliangua kicheko, kwa sababu hakutarajia swali kama hilo.

"Umeanza hivyo?"

"Ndiyo, shangazi yangu na baba yako baada ya kufunga ndoa si wamekufa pamoja na kuzikwa pamoja, mmoja kushoto, mwingine kulia?"

"Ndiyo unataka kusemaje?"

"Na mimi na wewe mmoja awe kushoto na mwingine kulia."

Alijihisi mwenye mkosi. Ilikuwa ni Jumamosi ya kwanza ambayo Shani hakwenda kwenye hoteli ya ABC.

Tayari alikuwa ameshapewa sumu ambayo angeiweka ama kwenye kinywaji au chakula na kumuanza kumuua taratibu na kufariki kiasi cha miezi mitatu au minne baadaye.

Mfukoni alikuwa ameshapewa kiasi cha Sh Milioni moja ambacho alishaanza kukitumia. Na alishaahidiwa kitita kingine kazi ikikamilika.

Siku hiyo hakuwa na raha kazini. Alikuwa akihudumia wateja, lakini akili yake ilikuwa mbali.


Mara nyingi muda ule msichana huyo anakuwa tayari ameshafika hapo kupata chakula cha mchana na kiywaji, kiasi kwamba hadi wahudumu walikuwa wameshamzoea.

Walimtambua kuwa ni binti ya mmoja wa vigogo wa maeneo hayo ya Mbezi Beach.

Hata hivyo walikuwa wakimshangaa kuwa na tabia ya kwenda peke yake, akiwa na gari aina ya Land Cruiser akiendesha mwenyewe.

Huwa hafuatani na mtu yoyote awe na kike au wa kiume.

"Vipi mbona leo kama unaumwa,




huna raha au kama kuna kitu kinakutatiza?"

Fikiri alishtuka kuulizwa swali hilo ambalo hakulitarajia.

"Siyo hivyo Seif, jana tumezinguana na demu wangu Zakia." Aliongopa.

Hakutaka mtu yoyote ajue kitu chochote, hata hisia yake tu kama hayuko vizuri kwa ajili ya kuficha chochote kitakachotokea mbele ya safari.

"Wewe nawe wanawake watakuua ndugu yangu, kila mwanamke unamtaka wewe, kila demu uwe naye wewe, utawamaliza?"

"Ndugu yangu Seif, hapa tuko kazini bwana, unanichanganya, hayo tutaongea baadaye." Fikiri alimjibu akiwa na lengo la kutaka kuuzima mjadala ule kwa uongo kwani ingawa ana tabia ya kupenda wanawake kupita kiasi, lakini si kweli kama alikuwa amegombana na mpenzi wake.

Aliyekuwa akimuwaza ni Shani. Hakuwa mpenzi wake. Alikuwa na kazi naye moja tu, ya kuumaliza uhai wake kwa kumuwekea sumu.

Alikuwa na wasiwasi na kudaiwa pesa alizopewa, lakini pia kutozipata zile zingine alizoahidiwa baada ya kumaliza kazi.

"Huyu demu noma, kama machale yamemcheza vile." Aliwaza.

Tangu aanze kazi mwaka mmoja uliopita, hajawahi kutomuona hata Jumamosi moja.

"Huu mkosi gani." Alijiambia mwenyewe.

Hakuwa na uhakika kama Jumamosi ijayo atakuja au hatokuja.

"Inawezekana anamwa wiki ijayo atakuja." Alijipa moyo.

Ni wiki moja sasa tangu aingie ofisini na kukutana na bosi wake Peter Mwambene, ambaye ni Mkurugenzi wa Usalama.

Waliongea mengi, lakini Eddy Kamal alimueleza kushangazwa na tukio la zaidi ya miezi sita iliyopita la mauaji ya bwana na bibi harusi, Patiyo na Grance Maumba kuwa mpaka sasa halina majibu.

Bosi wake alimwambia kuwa lilikuwa ni suala ya askari polisi ambao wako kwenye uchunguzi wa kubaini ni akina nani wamehusika.

Eddy alimweleza bosi wake kutoridhishwa na uchunguzi wa zaidi ya miezi sita wa tukio hilo ambalo liliitikisa nchi na hata kuwa gumzo kwenye vyombo vya habari vya kimataifa.

Aliiomba kesi hiyo itoke polisi na jalada akabidhiwe yeye kwa ajili ya kufanya upelelezi, lakini Mwambene alikataa na kusema bado ni kesi ndogo sana kwa wao kuichukua.

"Hata kama unasema bi harusi aliyeuawa ni shangazi yako, lakini haiondoi ukweli kuwa haya ni mauaji kama mengine yoyote yale ambayo polisi wanashughulika nayo. Ukumbuke Eddy, sisi tunashughulika na mambo makubwa. Matukio makubwa ya kuhatarisha usalama wa nchi, au wananchi. Hii ni jinai tu, waachie wenyewe polisi watashughulika nayo." Sauti ya mzee Mwambene ilirudia tena kwenye masikio yake na ilikuwa siku nne baada ya kuanza kazi rasmi akitokea masomoni Marekani.

Hata alipomwambia analiomba kwa ajili tu ya kutaka kuchangamsha akili na mwili, kwani ana miaka miwili sasa hajapata jalada lenye mkasa wowote unaotakiwa kufuatiliwa, ili kuchangamsha mwili na ubongo wake, lakini bado mzee Mwambene alikataa katakata. "Tutajidhalilisha" Alimwambia.

Akiwa amemaliza kujisomea moja ya vitabu vyake, majira ya saa tatu usiku, simu iliita.

Alipoiangalia alikutana na jina la Shani. Alijikuta anatabasamu bila sababu yoyote.

"Hujambo bibie?" Alianza kumsalimia.

"Sijambo, vipi siku ya nne hii rafiki yangu sijapata meseji yako wala simu. Ulinipigia na kunitumia meseji simu mbili tu alipotoka kwangu, lakini sasa naona unanisahau." Yalikuwa ni malalamiko ya Shani.

"Hapana sijakusahau. Siwezi kumsahau mrembo kama wewe. Ila siku ile nilipotoka kwako, siku mbili baadaye kuna mtu alinipa kibarua chake nimfanyie kwa wiki moja hivi."

"We nawe, mara huna kazi, mara nina kibarua, nikuelewe vipi?"

"Sina kazi, ina kuna wakati napata vibarua, tena vya muda mfupi tu, nikimaliza basi."

"Vibarua gani hivyo?" Shani aliuliza.

"Utavijua tu baadaye wala usiwe na haraka."

"Mimi kibarua changu nilichokupa mbona hukitaki?"

"Wala sijakikataa, nilikwambia tu cha kwako kikubwa na wala si kibarua, nipo kwenye harakati za kukipokea, usiwe na wasiwasi binamu."

"Hivi kwa nini?" Likuwa ni swali kutoka kwa Shani lililoulizwa na sauti ndogo na ya chini, tofauti na maongezi ya mwanzo, ambalo lilionekana kumshagaza kidogo Eddy.

"Kwa nini vipi?" Eddy naye badala ya kujibu aliuliza kwa mshangao.

"Hata mimi sielewi kwa kweli." Shali aliongeza mshangao kwenye akili ya Eddy.

"Hebu wewe niambie kwa nini?" Eddy alihamisha swali aliloulizwa na muulizaji, kutoka kwa muulizwaji kwenda tena kwa muulizaji."

"Ikipita siku hatujawasiliana inakuwa kama mwezi hivi. Hizi siku nne ambazo hatujawasiliana kwangu ilikuwa ni kama miaka minne." Shani alionekana kujibu swali ambalo alimuuliza Eddy, lakini kwa utaalam, hasa kutokana na kazi yake, alilirudisha kwake na kujikuta akijibu.

"Mimi tusipowasiliana siku moja nakuwa kama naumwa." Alijibu Eddy

"Muongo, mbona siku nne hukujanipigia wala kunitumia meseji?"

"Nilikwambia, nilikuwa kibaruani, huwa sipendi kuongea na wewe kijuujuu. Napenda niwe nimetulia. Tuongee maneno ya furaha, tukiwa tumetulia." Jibu hilo lilionekana kumtuliza Shani.

"Mmh, lakini wewe utakuwa ni sababu." Shani alisema na maneno hayo yalipenya hadi kwenye moyo wa Eddy, akasikia kusisimkwa na mapigo ya moyo kuongezeka.

"Hata mimi ninavyojisikia, sababu itakuwa ni wewe." Eddy naye alirudisha mapigo.

"Unajisikiaje?" Shani aliendelea kuwa mchokozi.

"Nasikia kama kuna kitu rohoni hivi."

"Kitu gani hicho?"

"Sijakijua, ila ngoja nikitafute, nikikipata nitakwambia, lakini ukweli ni kwamba nikikuona au kuwasiliana na wewe nasikia raha sana, ila nisipowasiliana na wewe au kukuona nakuwa kama yatima vile." Eddy naye ni kama alichokozwa hivi. Akawa anatema nyongo.

"Hahahaha haya bwana, kitafute hicho kitu, halafu uniambie." Shani alisema akionekana kufurahia maneno ya Eddy. Naye alihisi kitu kama msisimko mwilini, huku joto likiongezeka mwilini.

"Hiki kitu naona tukitafute wote. Nisaidie kukisaka. Tukikipata chetu wote." Alisema Eddy na alipomaliza alisikia kicheko kutoka upande wa pili wa simu. Maneno yalimfurahisha mno Shani. Eddy naye akajikuta anacheka. Wakaangua kicheko pamoja.

***Itaendelea Jumamosi***

# TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## NAFASI ZA KAZI

**NAFASI ZA KAZI YA DEREVA NA MAUZO** Mwenye uzoefu wa kuuza Maji. PIga simu namba : **0767 269677 saa za kazi**


NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE NASI

KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676


## KUPOTEA KWA VYETI



**PAUL JOSEPH** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S0605-0090** kilichotolewa na UHURU SEKONDARI mwaka 1999. Cheti cha kidato cha sita chenye index namba S0144-0543 kilichotoelwa na NSUMBA HIGH SCHOOL mwaka 2002.Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/MAG/RB/485350/2020.**

115791102

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI**
**IDAYA YA UHAMIAJI**

## OMBI LA URAIA WA TANZANIA



**FADZAI CHINYENGETERE**

Mwenye picha hapo juu, anaomba uraia wa Tanzania kwa Mh. Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi. Utaifa wake wa sasa ni ZIMBABWE. Nchi atokayo ni ZIMBABWE. Yupo hapa nchini tangu 2019. Kwa yeyote mwenye taarifa/sababu za kwanini mwombaji asipewe Uraia wa Tanzania, atume taarifa ya maandishi kwa Kamishna Jenerali wa Uhamiaji S.L.P 512, Dar es salaam. Kumb Na. DN. 352803

FOR: COMMISSIONER GENERAL OF IMMIGRATION

115789402

## KUPOTEA KWA KADI GARI

**DOMINICK ELIUDI MOLLEL** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 892 ARM.** Engine No. **WA1600419810.** Chassis No. **CD24423050.** Jina la umiliki ni **BILIGWA LUDOVICKY KATAMAGO.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **ARU/ARU/RB/476082/2020.** Au piga simu No. **0753180901.**

115790602

## KUPOTEA KWA OFFA YA KIWANJA

**JUMA BAKARY MSANGI** MKAZI WA NDALA MANISPAA YA SHINYANGA. ANATANGAZA KUPOTELEWA NA OFFA YAKE YA KIWANJA **NAMBA 633 KITALU "HH"** AMBAYO ILIPOTEA MWEZI MEI MWAKA 2020 MAENEO YA SHINYANGA. KWA YEYOTE ATAKAE IONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHOPO KARIBU AU AWASILIANE JUMA BAKARY MSANGI KWA SIMU NAMBA **0759-630742 AU 0789-476744 RB NAMBA SHY/RB/2020, CONTROL NAMBA 9910812809075**

115791002

**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF DODOMA AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 41 OF 2020**

**In the matter of the Estate of the late REBECCA ISAACK NGOMUO of Dodoma Municipality/ City**

**AND**

**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY SARAH**

**I. NGOMUO AND MARCUS RASHID KILAMA**

**GENERAL CITATION**

**(RULE 75 PROBATE RULES GN 369 OF 163)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 10 Day of July 2020.

Date at Dodoma this 25 Day of JUNE 2020.

RESIDENT MAGISTRATE

115791302


## KUPOTEA KWA CHETI



**IDIFONS P. ADRIAN** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S.2857/0066** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia MAKI SEKONDARI mwaka 2016. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/KIG/RB/455768/2019.**

115791402

## KUPOTEA KWA VYETI



**PELLO KESILET** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.0978/0092** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia DIGODIGO SEKONDARI mwaka 2010. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/CHA/RB/420912.**

115790902

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM II**

**(S.M.M 1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**

**KATIKA MAHAKAMA YA WILAYA DODOMA MJINI**

**USIMAMIZI WA MIRATHI NA. 58 OF 2020**

**Ombi la FRIDA EMMANUEL kuteuliwa msimamizi wa mirathi ya marehemu EMMANUEL GAUDENCE MWIKUKA**

watu wote wanaodai kuwa na mahusiano wowote na mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnano tarehe 1/7/2020 kabla huyo mwombaji kuteuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia wa Marehemu upo mahakamani waweza kukaguliwa Tarehe….23/06/2020

Sahihi ya Hakimu

115791602

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**FRANK TITHO MBILINYI** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 174 BYP** SCANIA. Engine namba 4015777. Chassis namba **04333950.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **DAR/OST/RB/481956/2020.**

115790702

## KUBADILISHA UMILIKI

**SAMUEL TYALLAMBULLA** MAKALLA WA **S.L.P 1464** DODOMA ANAOMBA KWA MENEJA TRA DODOMA KUBADILISHA UMILIKI WA GARI TOYOTA **SURF T 683 ABK** KUTOKA KWA NGUGU MAKORANI JABIR JOSHUA KWENDA KWA NDUGU SAMUEL TYALLAMBULLA MAKALLA WA **S.L.P 1464 DODOMA.** ***YEYOTE MWENYE PINGAMIZI ATOE NDANI YA SIKU 14 KUANZIA TAREHE YA TANGAZO***


Kwa Habari Motomoto

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
MWANGA WA JAMII



TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.



# SOLSKJAER

## AJIPANGA KWA USAJILI MPYA

**MANCHESTER, England**

KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer, amesema atangia sokoni kusajili kama kutakuwa na mchezaji wa maana anayeuzwa kwa bei inayoridhisha.

Kocha huyo amekuwa kwenye kikosi cha United kwa miezi 18 na ameshashuhudia dirisha moja la usajili wa majira ya kiangazi.

United imetumia karibu pauni milioni 150 kusajili wachezaji watatu na licha ya kudaiwa kuwapo na mtikisiko wa kiuchumi uliosababishwa na janga la corona, kocha huyo anaamini kuna uwezekano wa kuendelea kuwekeza tena mara dirisha la usajili litakapofunguliwa.

Solskjaer ameshaweka bayana vigezo vyake vya usajili huku kwa wakati huu akiweka mkazo wa timu hiyo kufuzu kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Anafahamu kikosi chake kimeachwa mbali kiubora na mahasimu wao Manchester City na Liverpool, hivyo suala la kunasa vichwa vya maana halikwepeki.

Kwa kipindi cha karibuni, miamba hiyo ya Old Trafford imekuwa ikihusishwa na mastaa kama Jadon Sancho, James Maddison, Jack Grealish, Kai Havertz na Kalidou Koulibaly.

"Manchester City na Liverpool, kwa misimu miwili iliyopita, wameweka viwango kuwa juu kwenye ligi," alisema Ole.

# MEUNIER AKAMILISHA USAJILI DORTMUND

**DORTMUND, Ujerumani**

BEKI wa kimataifa wa Ubelgiji, Thomas Meunier, amesaini mkataba wa miaka minne kuichezea Borussia Dortmund, baada ya kuwa mchezaji huru kule Paris Saint-Germain.

Mlinzi huyo wa kulia mwenye umri wa miaka 28, alitumia misimu minne akicheza kwa mabingwa hao wa Ufaransa, akishinda mara tatu taji la Ligi Kuu maarufu Ligue 1, Kombe la Ligi na Kombe la Ufaransa.

Hata hivyo, yeye ni mmoja wa wale wanaoondoka hapo PSG baada ya mikataba yao kumalizika mwezi huu pamoja na Edinson Cavani na Thiago Silva na haraka amepata sehemu mpya ambayo ni kwenye Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, kwa kujiunga na Dortmund, ambao atajiunga nao kwa ajili ya msimu ujao.

"Borussia Dortmund wanacheza soka ninalohitaji kucheza: la kuvutia, nguvu na akili," amesema mlinzi huyo wa zamani wa Brugge, Meunier akinukuliwa na tovuti ya klabu hiyo.

"BVB inajulikana kuwa na mashabiki wenye hamasa kubwa na hata tulipokutana nao kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya pale Paris na dimba la Signal Iduna Park, kwa hakika ilinivutia kufanya uamuzi wangu.

"Malengo yangu ni kama ilivyokuwa nilipocheza Bruges na Paris, ningependa kushinda mataji na Dortmund."

Meunier, ambaye ameichezea Timu ya Taifa ya Ubelgiji mechi 40, anaweza kwenda kuziba pengo la Achraf Hakimi anayerudi Real Madrid baada ya kucheza kwa mkopo hapo kwa misimu miwili.



# NBA KUENDELEA TENA JULAI 31

**NEW YORK, Marekani**

MSIMU wa Ligi Kuu ya Kikapu ya Marekani (NBA), wa 2019/20 utarejea tena kuanzia Julai 31, mwaka huu wakati timu 22 zitakapokuwa zikishindana katika mashindano yatakayofanyika Orlando na Florida.

Mechi hizo zitakuwa kwa ajili ya kumalizia msimu wa ligi hiyo baada ya kusimama kutokana na mlipuko wa virusi vya corona.

Kuendelea kwa msimu huo kuliidhinishwa na makubaliano na wamiliki wa timu na huku kukiwa na klabu moja tu iliyopiga kura ya hapana dhidi ya kurejea kwa msimu, ambayo ni Portland Trail Blazers.

Mashabiki wa mpira wa kikapu wanatarajia kurudi kwa Chama na mashindano ya timu 22 yatakayomtafuta na kumtangaza bingwa.

Mashindano hayo ya mpira wa kikapu huko Orlando si ya pekee ya mchezo wa kulipwa yanayofanyika katika jiji hilo, kwa mujibu wa Real Soccer 365, ligi kubwa za soka pia zinaweza kurejea kwenye jiji hilo na kuhitimisha mashindano kwa kutumia muda mfupi.

Mashindano ya NBA yatafanyika kwenye Hoteli ya Walt Disney World ambayo yatakwenda mpaka Oktoba.



## HABARI MICHEZO




# LIVERPOOL

## NA MIAKA 30 YA MATESO UBINGWA WA EPL

**LONDON, England**

JURGEN Klopp amesema ushindi Liverpool wa Ligi Kuu England umeongeza ndoto yake na hisia kubwa zaidi kama kocha wa Wekundu hao kusheherekea kumaliza ukame wa kuwania taji hilo.

Liverpool ilimaliza miaka 30 ya kusubiri kulibeba Kombe la Ligi Kuu England, EPL, shukrani kwa Manchester City kufungwa mabao 2-1 na Chelsea Alhamisi usiku.

Kombe hilo ni la 19 kwa Liverpool na la kwanza tangu msimu wa 1989/90.

Klopp amekuwa kocha wa kwanza wa Liverpool kuwapa kombe hilo vijana hao wa dimba la Anfield tangu mwaka 1990, huku zikiwa zimesalia mechi saba kumalizika kwa msimu wa 2019/20.

Alipoulizwa kuhusu hisia zake baada ya kutwaa kombe hilo, Klopp - ambaye alichukua mikoba ya kuinoa timu hiyo kutoka kwa Brendan Rodgers mwaka 2015, aliiambia tovuti ya Liverpoolfc.com: "Hapana, siwezi kuzungumza sana kuhusu hili, kwani naweza kujikuta nikianza tena kulia.

"Hii ni zaidi ya mafanikio, kwa hakika kabisa furaha yangu imezidi kikomo; Sijui imechanganya kila kitu - ninashukuru sana, nina furaha sana, najisikia fahari kubwa.

"Nisingeweza kujisikia fahari bila vijana hawa. Tuliuangalia mchezo pamoja usiku, tulijua kwamba inaweza kutokea au isitokee, hatukujua.

"Tulitaka kucheza soka na kila mmoja alikuwa na furaha kwamba tuliruhusiwa kuendelea na soka - na hiki kilichotokea sasa kwa hakika kabisa ni kitu kikubwa mno kwetu.

"Wakati tulipoanza kuhesabu sekunde tano zilizobakia kwenye mchezo ule, mwamuzi aliongeza sekunde zaidi, hivyo tukatakiwa kuangalia tena pasi mbili au tatu!

"Halafu ndio ikatokea Manchester City wamepoteza. Siwezi kuelezea furaha niliyokuwa nayo. Kwa uhakika kabisa ulikuwa wakati mzuri na bora zaidi katika maisha yangu.

"Haraka baada ya mchezo huo, sikuamini nilijihisi kama nipo sehemu tofauti kabisa katika maisha yangu.

"Tulikaribia wakati kama huo miaka mitatu iliyopita na mwaka jana tulikaribia sana kulibeba taji, lakini mambo yakaenda tofauti kabisa, ... kwa kile walichokifanya vijana wangu kwa kipindi cha miaka miwili na nusu iliyopita, kwa hakika kabisa wanastahili hiki.



**KLOPP**

**amekuwa kocha wa kwanza wa Liverpool kuwapa kombe hilo vijana hao wa dimba la Anfield tangu mwaka 1990, huku zikiwa zimesalia mechi saba kumalizika kwa msimu wa 2019/20.**

"Kiwango walichokionyesha ambacho hakikushuka, kwa hakika kabisa ilitakiwa kupata kitu kama hiki, na sasa tumekamilisha ndoto yetu ya muda mrefu."

Klopp, ambaye pia aliiongoza Liverpool kutwaa ubingwa wa Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu uliopita, aliongeza: "Miaka 30 iliyopita... nilikuwa na umri wa miaka 23, hivyo sikuwahi kufikiria kuja kushinda Kombe la Ligi Kuu na Liverpool, kwa uhakika kabisa sikuwa na wazo hilo."

**REKODI**

Kushinda taji hilo ndio lililokuwa lengo la Liverpool ambayo ilikuwa imesubiri kwa muda mrefu ili kutawazwa mabingwa tena, baada ya kushinda taji hilo mara 11 kati ya 1973 na 1990.

Lakini baada ya ufanisi huo, huenda mambo yakaimarika zaidi, na kuvunja rekodi ya pointi 100 iliyowekwa na klabu ya Manchester City.

Timu hiyo ya Klopp imefanya kampeni kali katika historia ya ligi hiyo, kwa kujipatia pointi 86 na rekodi ya kushinda mechi 28, sare mbili na kufungwa mara moja katika mechi zao 31.

Hivyo ndivyo walivyotawala, na katika wakati mmoja waliongoza jedwali la ligi wakiwa na pointi 25- uongozi uliovunja rekodi na wa pili katika historia ya ligi hiyo. Ushindi wao wa taji hilo la ligi msimu huu ndio wa mapema katika rekodi, huku wakiwa wamesalia na mechi saba.

Huo sio ushindi wa mapema kwa tarehe, ni kwa sababu ya kusitishwa kwa ligi kati ya Machi na Mei kutokana na mlipuko wa virusi vya corona.

Ushindi huo wa Liverpool unawakilisha wakati muhimu kwa mashabiki wake, waliokuwa wakizoea ushindi kati ya miaka ya 1970 na 1980, ikiwamo ushindi wa msimu wa 1972/73 na 1990/91 ambapo walishindwa kumaliza katika nafasi ya kwanza au ya pili katika ligi hiyo.

Hata hivyo, hawajakosa kushinda taji katika kipindi hicho cha miaka 30, wakishinda Kombe la FA, makombe manne ya Kombe la Ligi, Kombe la Ligi ya Mabingwa Ulaya mara mbili-la mwisho wakishinda chini ya Klopp - pamoja na makombe matatu ya Super na moja la Klabu Bingwa ya duniani.

HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# JUVENTUS YAJITOSA KWA AUBAMEYANG

Itatakiwa kujipanga kuwania saini ya straika huyo ambaye pia anawindwa na Barca, Madrid, United...

**TURIN, Italia**

KLABU ya Juventus imeingia kwenye vita ya kuwania saini ya straika wa Arsenal, Pierre-Emerick Aubameyang, taarifa mbalimbali zimeandika.

Nahodha huyo wa The Gunners, ambaye bado hajafikia makubaliano ya kusaini mkataba mpya wa kuendelea kubakia Emirates, pia anatajwa kuzivutia Barcelona, Inter Milan, Real Madrid na Manchester United.

Lakini le10sport.com limeandika mabingwa na vigogo hao wa Serie A wameanza kufuatilia taarifa za mshambuliaji huyo kuangalia uwezekano wa kumsajili.

Mkataba wa sasa wa straika huyo unatarajia kumalizika mwakani na Arsenal inaweza ikampoteza kirahisi kana itashindwa kumshawishi kusaini mkataba mpya baada ya kutokubaliana na vipengele vipya.

Lakini taarifa nyingine zinasema uwezekano wa mshambuliaji huyo kusaini mkataba mpya upo wazi na bado inaendelea kufanyia kazi mchakato huo.

Barcelona na Inter Milan ni timu ambazo zimeshatangaza nia ya kumsajili mchezaji huyo wa Timu ya Taifa ya Gabon. Hata hivyo usajili wake utategea na hatima ya mshambuliaji wa Inter, Lautaro Martinez, ambaye anahusishwa kujiunga na klabu ya LaLiga.

Kama atafanikiwa kutua Katalunya, kikosi cha Antonio Conte kinahitaji kumsajili Aubameyang ili kuziba nafasi itakayokuwa imeachwa wazo, lakini klabu hiyo ya Italia itatakiwa kupambana kuhakikisha inaweza kumlipa mshahara atakaohitaji nyota huyo.

Wiki iliyopita, Mikel Arteta, alikaririwa akisema anaamini mazungumzo kati ya The Gunners na mshambuliaji huyo mwenye umri wa miaka 31, yamefikia hatua nzuri ingawa tayari kuna klabu nyingine zimeonyesha kumwania.

Aubameyang amefunga mabao 20 katika mashindano mbalimbali msimu huu na ni mchezaji muhimu ambaye anamsaidia Arteta kuamini bado wana nafasi ya kumaliza kwenye 'Top Four' katika msimu ujao.

Jumatano iliyopita, klabu hiyo tayari imetangaza David Luiz amesaini mkataba mpya wa mwaka mmoja wa kuendelea kubakia Emirates huku Cedric Soares na Pablo Mari waliokuwa hapo kwa mkopo, wakipewa mikataba ya kudumu.

## KWA UFUPI

**ARTHUR AKARIBIA JUVENTUS**
KIUNGO wa Barcelona na Timu ya Taifa ya Brazil, Arthur, ambaye ana umri wa miaka 23, anakaribia kujiunga na Juventus kwa dau la pauni milioni 72.5 ***(Sky Sports)***

**PJANIC KUTUA BARCELONA**
KIUNGO wa Juventus na Timu ya Taifa ya Bosnia, Miralem Pjanic, ambaye ana umri wa miaka 30, anajipanga kuhamia Barcelona kwa dau la pauni milioni 54.25 dirisha la usajili la majira ya joto litakapofunguliwa. ***(Sky Sports)***

**ROMA YAMSAJILI PEDRO**
WINGA Mhispania, Pedro, ambaye ana umri wa miaka 32, anatarajia kujiunga na Roma kwa mkataba wa miaka miwili baada ya mkataba wake na Chelsea kumalizika mwishoni mwa msimu huu. ***(Sky Sports)***

**BAYERN YANAWA MIKONO**
BAYERN Munich haitajiunga na Manchester United katika mchakato wa kuwania saini ya kiungo wa Birmingham, Jude Bellingham (16), ambaye ameonyesha kuvutiwa na Borussia Dortmund. ***(Bild, via Sun)***

**WILLIAN ALITAKIWA ARSENAL**
ARSENAL ilikuwa tayari kumpa mkataba wa malipo ya mshahara wa pauni 250,000 kwa wiki mshambuliaji wa Chelsea Mbrazil, Willian (31), kipindi kabla ya janga la corona halijaingia. ***(Mirror)***

**RAYMOND ANUKIA LEEDS**
LEEDS United iko katika hatua nzuri za mazungumzo ya kumsajili kiungo wa England, Jadan Raymond (16), baada chipukizi huyo kukataa kusaini mkataba wa kwanza na Crystal Palace. ***(Athletic - subscription needed)***

**MOURINHO ATAKA WATANO**
KOCHA wa Tottenham, Jose Mourinho, amemwambia Mwenyekiti wa timu hiyo, Daniel Levy anahitaji wachezaji watano wapya katika dirisha la majira ya joto, lakini Spurs itatakiwa kujipanga kusajili nyota wa mkopo au waliokuwa huru. ***(90min)***

**RODGERS AMFUNDA MADDISON**
KOCHA Brendan Rodgers amemweleza, James Maddison (23) kuwa Leicester ndio sehemu sahihi kwake baada ya kuwapo kwa tetesi za kiungo huyo wa Timu ya Taifa ya England anatakiwa na Manchester United. ***(Leicester Mercury)***

**RODRIGUEZ NJIA MOJA**
WINGA wa Real Madrid na Timu ya Taifa ya Colombia, James Rodriguez (28), ambaye amebakisha mwaka mmoja katika mkataba wake, bado amefungua milango ya kujiunga na Napoli. ***(AS - in Spanish)***

**ARSENAL, MILAN VITANI**
ARSENAL na AC Milan ziko katika mazungumzo na kiungo wa Red Bull Salzburg, Dominik Szoboszlai ambaye ana umri wa miaka 19, huku pia Paris St-Germain inatajwa kumwinda chipukizi hiyo raia wa Hungary. ***(Express)***

**ORTA KUTUA RED BULL**
MABOSI wa Kituo cha Soka cha Red Bull wamemtaja Mkurugenzi wa Soka wa Leeds United, Victor Orta, ndiye anayefaa kuchukua majukumu ya kiufundi kwenye klabu yao. ***(Independent)***

HABARI MICHEZO

# MWAMNYETO AFUNGUKA KUSUASUA KWA COASTAL

**Na Saada Akida**

NAHODHA na beki wa kati wa Coastal Union, Bakari Mwamnyeto, amesema kikosi chao kinapambana kuhakikisha wanapata matokeo mazuri katika michezo yote iliyobakia ili kufikia malengo ya kumaliza katika nafasi tano za juu kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mwamnyeto alisema mechi zote za Ligi Kuu Tanzania Bara ni ngumu na changamoto imeongezeka zaidi wanapokutana na klabu zilizoko kwenye hatari ya kushuka daraja.

Beki huyo alisema wanalazimika kuongeza juhudi zaidi katika mechi zilizosalia bila kujali wanacheza na timu gani, kwa sababu wanahitaji kuona wanafikia malengo yao.

"Ligi imerejea na ushindani mkubwa, kila timu inapambana kushinda mechi zake, benchi la ufundi limefanyia kazi upungufu wetu ikiwamo kuungana vizuri kwa timu baada ya wachezaji kutoka kufanya mazoezi binafsi wakati wa kipindi cha janga la corona,"alisema Mwamnyeto.

Beki huyo alisema licha ya makosa madogo yaliyopo, kikosi chao kipo vizuri lakini wanatakiwa kuendelea kujituma ili kufikia malengo waliyojiwekea hapo awali wakati msimu huu unaanza.

"Lazima tupambane na kucheza kwa nidhamu ya hali ya juu, pia tunatakiwa kuwaheshimu wapinzani wetu tunaokutana nao, iwe nyumbani au ugenini," Mwamnyeto alisema.

Nahodha huyo aliongea wamepoteza alama tano na kupata pointi mbili katika michezo mitatu iliyopita jambo ambalo limepunguza kasi yao.

Coastal Union yenye pointi 48, ipo katika nafasi ya tano kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara na leo inatarajiwa kuikabili Alliance FC kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jijini, Mwanza.



Wachezaji wa Boma FC, wakifanya mazoezi kwenye Uwanja wa Karume jijini, Dar es Salaam, kujiandaa na michezo mbalimbali ya Ligi Daraja la Kwanza inayoendelea hapa nchini. **PICHA : JUMANNE JUMA**

# Kipanga yafikiria ubingwa Zanzibar

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

TIMU zinazoshiriki Ligi Kuu Zanzibar zimekuwa zikijiimarisha tayari kuendelea na mbio za kuwania ubingwa wa ligi hiyo ambayo inatarajia kuendelea tena kuanzia Julai Mosi, mwaka huu, imefahamika.

Ligi hiyo ambayo hutoa mwakilishi wa Zanzibar katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika, ilisimama tangu Machi, mwaka huu ili kujikinga na ugonjwa wa corona.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu Msaidizi wa Kipanga, Maulid Othman, alisema timu yao inafanya mazoezi kila siku na wachezaji wanafuata vema programu zinazotolewa na benchi la ufundi la timu hiyo.

Othman alisema baada ya serikali kuruhusu mazoezi ya pamoja, wachezaji wao wameimarika na wako tayari kuendelea kushindana kuwania pointi tatu katika kila mechi watakayocheza.

"Katika kuhakikisha tunakuwa imara, kikosi chetu kimecheza michezo miwili ya kirafiki dhidi ya timu za Ligi Kuu Zanzibar," alisema kiongozi huyo.

Alisema mchezo wa kwanza wa kirafiki walipata ushindi wa bao 1-0 dhidi ya KVZ na baadaye wakalazimishwa sare goli 1-1 dhidi ya Chuoni.

Katika msimamo wa Ligi Kuu Zanzibar, Kipanga ipo kwenye nafasi ya sita ikiwa imebakisha michezo tisa kumaliza msimu huu wa 20019/20.

## Tanzania bado yaiwaza Uganda

**Na Saada Akida**

SHIRIKISHO la Soka Tanzania (TFF), limesema hivi karibuni litatoa tamko kuhusiana na rufaa waliyokata dhidi ya Uganda, ambao inadaiwa kutumia wachezaji wakubwa katika mashindano ya soka ya wanawake ya umri chini ya miaka 17, imeelezwa.

Katibu Mkuu TFF, Wilfred Kidao, alisema kuwa rufaa yao imefikia mahali pazuri na wanaamini ndani ya siku chache zijazo, watapokea uamuzi kutoka katika Shirikisho la Soka la Kimataifa (Fifa).

Kidao alisema mchakato huo unaendelea vizuri na wamejulishwa hatima ya rufaa hiyo itajulikana kabla ya ratiba mpya ya mashindano haijatolewa.

Alisema kwa sasa hawawezi kusema chochote kwa sababu suala hilo lipo katika vyombo vya sheria na wanahitaji kuwa na subira kusubiri uamuzi rasmi.

"Wiki ijayo nitatolea tamko suala zima la rufaa yetu hiyo, hapa kati tulishindwa kutokana na sababu ya janga la corona, pia suala hilo lipo chini ya mikono ya vyombo vya sheria, tusubiri majibu yao ili tuwaeleze Watanzania majibu yaliyofikiwa," alisema Kidao.

Aliwataka wadau wa soka la wanawake kuwa na subira juu ya hatima ya rufaa yao, na wanaamini uamuzi utafanyika kwa haki.

## Wawili waripoti Marsh Queens

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Marsh Queens, Aaron George, amesema timu yake inakabiliwa na ukata na iko katika mazingira magumu ya kujiandaa na mechi za Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania, ambao inatarajiwa kuendelea tena kuanzia kesho hapa nchini.

George aliliambia gazeti hili hali hiyo inampa changamoto katika kutekeleza programu zake za mazoezi na kurudisha nyuma mipango na mikakati ya ushindi.

Kocha huyo alisema mpaka sasa ni wachezaji wawili tu ndio wamerejea kwenye kambi ya timu na hivyo anashindwa kuwapa mazoezi yanayostahili.

"Hali ya uchumi ni mbaya sana, kwa viongozi kushindwa kuwatumia fedha za nauli wachezaji wao ili warejee katika sehemu ya kazi kwa ajili ya kuendelea na mazoezi ya kumalizia msimu," alisema kocha huyo.

Alisema hata kama wachezaji hao watafanikiwa kurejea, timu yake itakuwa katika wakati mgumu wa kushindana kutokana na kukosa muda mzuri wa kuwaandaa.

"Bado haijulikani wachezaji wengine watawasili lini hapa Mwanza, hali ya uchumi sio nzuri kabisa, ukifuata wadau wanasema hawana kitu, wanakwambia corona imeharibu kila kitu, sijui tutafanya nini na muda umekwenda," George alisema.

Marsh Queen itashuka kuwakabili majirani zao TSC katika mechi ya Ligi Kuu Wanawake itakayochezwa Jumatatu kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jijini, Mwanza.

Michezo

Jumammosi Juni 27, 2020

Nipashe



Liverpool na miaka 30 ya mateso ubingwa wa EPL

HABARI UK 21



Wachezaji wa Liverpool, Fabinho (kushoto), na Roberto Firmino wakishangilia ubingwa wa Ligi Kuu England kwa timu yao msimu wa 2019/20 baada ya Manchester City kupokea kichapo cha mabao 2-1 kutoka kwa Chelsea juzi usiku. Stori kamili ukurasa wa 21. **PICHA: MTANDAO**

# YANGA DIMBANI IKIIWAZA SIMBA

Ni katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Ndanda leo, huku Azam ikiwa ugenini Musoma...

**Na Somoe Ng'itu**

WAKATI safari ya kuwania taji la Ligi Kuu Tanzania Bara ikielekea ukingoni, vinara wa ligi hiyo, Simba, wanaweza kutawazwa mabingwa wapya endapo Yanga na Azam FC watapoteza mechi zao za wakiwa kwenye viwanja tofauti hapa nchini.

Yanga itawakaribisha Ndanda FC kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam, wakati Azam FC iliyoko Musoma mkoani Mara itawavaa wenyeji Biashara United.

Yanga yenye pointi 57 ikishinda mechi ya leo, na michezo mingine sita itakayofuata, itafikisha pointi 78 wakati Azam wenyewe wakishinda mechi zote zilizosalia watafikisha pointi 79, wakati Simba inayoongoza ligi ina pointi 78 mkononi.

Katika mechi ya leo, Yanga itaendelea kuwakosa wachezaji wake wa kimataifa wawili, Bernard Morrison na Lamine Moro, ambao wamefungiwa na Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), kutokana na makosa tofauti.

Akizungumza na gazeti hili, Kocha Mkuu wa Yanga, Luc Eymael, alisema kila mechi kwao ni sawa na fainali na watashuka uwanjani leo kuikaribisha Ndanda wakiwa na mipango tofauti.

"Kuna makosa mbalimbali tumefanya katika mechi zetu tatu zilizopita, lakini kesho (leo), tutakuwa tofauti, tunahitaji pointi tatu tu na si matokeo mengine, nina matumaini tutapata ushindi, ili tutimize malengo yetu," Eymael alisema.

Naye Ofisa Mhamasishaji wa timu hiyo, Antonio Nugaz, amewataka mashabiki wa Yanga wawe na subira na kuendelea kuishangilia timu yao ili ipate ushindi ili kuendelea kuwania nafasi ya pili wanayoifikiria.

"Tayari mwalimu wetu, (Eymael) ameshayafanyia kazi matatizo na namna timu itakavyokuwa inapata magoli, licha ya changamoto zilizojitokeza katika mechi mbili zilizopita, tuungane kwa pamoja," Nugaz alisema.

Kocha wa Ndanda, Abdul Mingange, aliliambia gazeti hili kikosi chake kitaingia uwanjani kuwakabili Yanga tahadhari ili kuondoka na pointi.

Mingange alisema katika mechi hiyo kila upande inataka matokeo na wamekuwa na ushindani kila wanapokutana kuanzia timu yake ilipopanda daraja.

Aliongeza wachezaji wa Yanga hawakati tamaa hadi mwisho wa mchezo, hivyo wataingia uwanjani wakiwa makini zaidi.

"Mimi na wachezaji wangu tumeshazungumza tunahitaji pointi, katika mechi hizi tatu tunahitaji hata pointi moja, tunajua Yanga pia inahitaji hata pointi moja, tunawaheshimu na tunafahamu ni timu kubwa, ina wachezaji wazuri na wanaolipwa vizuri," Mingange alisema.

Kipa wa Ndanda FC, Ally Mustapha, alisema timu yao inaundwa na wachezaji mchanganyiko, hivyo wataingia uwanjani wakiwa na malengo ya kusaka ushindi tu.

"Ni timu kubwa, tunawaheshimu Yanga na wakiwa nyumbani wana faida yao, tunawaheshimu lakini Jumamosi tutaingia kusaka matokeo," Barthez, kipa wa zamani wa Simba na Yanga alisema.

Mechi nyingine za Ligi Kuu Bara zitakazochezwa leo ni Ruvu Shooting itakayowakabili Namungo wakati Alliance itawavaa Coastal Union huku Mwadui ikiwapokea Mtibwa Sugar na Mbeya City itapambana na JKT Tanzania.

Kagera Sugar ambayo msimu huu imezinduka mapema itawakaribisha KMC FC ambayo iko kwenye hatari ya kushuka daraja endapo itaendelea kuvurunda.

## REKODI ZATAWALA PRISONS VS SIMBA

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI Prisons ikitarajiwa kuipokea Simba kwenye Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya kesho Jumapili, timu hiyo inaongoza kwa kutoa sare nyingi kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu hadi kufikia jana.

Prisons inayokamata nafasi ya 10, ikiwa na pointi 42 kwa mechi 31 ilizocheza, imetoa sare mara 15 mpaka sasa ikiwa ni rekodi ya juu ambayo haijafikiwa na timu yoyote msimu huu mpaka sasa.

Maafande hao watashuka dimbani kucheza dhidi ya Simba ambayo nayo ndiyo timu iliyotoa sare chache zaidi kwenye ligi hiyo mpaka sasa, ikiwa pia ndio mabingwa watetezi.

Simba ina sare tatu tu kwenye Ligi Kuu mpaka sasa ambazo ni za mabao 2-2 dhidi ya Yanga, mzunguko wa kwanza, sare ya bila kufungana kati ya timu hizo mbili (Simba na Prisons), katika mechi ya mzunguko wa kwanza, na ile ya bao 1-1 dhidi ya Ruvu Shooting.

Katika mechi 31 ambazo imecheza, Prisons imeshinda mechi tisa, sare 15 na kupoteza michezo saba.

Timu hiyo inayomilikiwa na Jeshi la Magereza, wanafuatiwa na Yanga ambao mpaka sasa imetoa sare mara 12 na kuwa ni moja kati ya timu yenye sare nyingi msimu huu.

Yanga inakamata nafasi ya tatu kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara ikiwa na pointi 57, imecheza michezo 31, ambapo wameshinda mechi 15, sare 12 na kupoteza mechi nne wakati Ndanda na JKT Tanzania zinakamata nafasi ya tatu, kila moja ikiwa imetoa sare mara 11.

JKT Tanzania inayokamata nafasi ya sita kwenye msimamo wa ligi ikiwa na pointi 47, imeshinda mechi 12, sare 11 na kupoteza mechi nane, huku Ndanda ambayo leo inacheza dhidi ya Yanga, imeshinda mechi nane, sare 11 na kupoteza mechi 12, ikiwa na pointi 35, kwenye nafasi ya 15 ya msimamo wa ligi.

Timu nne za Namungo, Mwadui, Biashara United na Mtibwa Sugar zinafuatia kwa kila moja kutoa sare mara 10.

Namungo ipo juu ya hizo, ikishika nafasi ya nne kwa pointi 55, Biashara United ikiwa kwenye nafasi ya tisa kwa pointi 43, Mtibwa Sugar ikiwa kwenye nafasi ya 12 kwa pointi 37 na Mwadui nafasi ya 13 kwa pointi hizo hizo 37.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >